**JELA** miaka minane kuua kwa kuingilia ugomvi mama, mtoto



UKURASA 10

**MAJAHAZI** yanaswa na madumu 925 ya mafuta ya magendo

UKURASA 4



BUFE

Nipashe

MARSHALL MBISE
Mama mwenye ulemavu miaka 23 katika mapambano magumu kujikimu

Mshika usukani wa awamu ya sita anavyovaa viatu uchumi vya JPM

UKURASA 11


# Nipashe

Ijumaa Juni 9, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581336

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US


## Sarakasi zazidi kunoga CWT

UKURASA 15

# Uendeshaji wa bandari moto

**MBOWE,** Zitto wanena; Spika, TPA watoa ufafanuzi... *Endelea Uk. 2*



Kiongozi wa ACT Wazalendo, Zitto Kabwe

Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe

Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Plasduce Mbossa

Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson

## Wazazi wajijazia ripoti kadi kliniki pasipo kuhudhuria kituo cha afya

UKURASA 3



**MICHEZO** **MIQUISSONE ATAJWA KUREJEA SIMBA SC** UK. 24

**KATUNI** UK. 6



# Uendeshaji bandari moto

**Na Restuta James**

WAKATI mjadala kuhusu uendeshaji wa bandari ukiendelea kupamba moto, Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari (TPA), Plasduce Mbossa, amesema 'hakuna mkataba wa miaka 100 na bandari haijauzwa.'

Pia amesema hakuna mkataba wowote kati ya TPA na DP World kama inavyodaiwa na badala yake kuna mkataba wa awali kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai.

Jana katika mazungumzo na Kituo cha Runinga cha Clouds jijini Dar es Salaam, Mbossa alisema: "Mtu anapokwambia (bandari) imeuzwa, lazima akueleze utaratibu... mtu anaondoka nayo au anamiliki? Kwa hiyo, niseme hakuna suala la kuuza bandari."

Alisema TPA imekuwa ikishirikiana na kampuni zingine, akitolea mfano wa mkataba uliomalizika mwishoni mwa mwaka jana kati yake na Kampuni ya Hutchison kutoka Hong Kong, iliyokuwa inaendesha gati ya makasha kupitia TICTS kwa miaka 22.

"Haikuwa imeuziwa bandari na ndiyo sababu imeondoka Desemba 2022, walikuwa wamekodishwa. "Hizo allegations (madai yanayohusu ubinafsishaji wa bandari ninaamini kwamba zinalenga kudhoofisha jitihada ambazo serikali inazifanya kuongeza ufanisi katika bandari yetu. Na mimi ninasema kwamba tuko katika ushindani mkali sana."

Mbossa alifafanua kuwa kwa sasa kuna mkataba wa Intergovernmental Agreement (IGA) baina ya Serikali ya Tanzania na UAE, unaoeleza eneo la ushirikiano ikiwamo mafunzo, Tehama na uendelezaji na uendeshaji wa bandari.

Alisema kuwa pamoja na mambo mengine, mkataba unaelekeza maeneo ya ushirikiano yatatiwa saini mikataba mingine baina ya pande mbili ambazo ni TPA na DP World.

"Baada ya Bunge kuridhia kutakuwa na mikataba ya utekelezaji wa shughuli husika kwa kuzingatia sheria, kama vile mikataba ya TEHAMA, mafunzo, uendeshaji na uendelezaji ambapo kwa sasa mikataba hiyo bado haijatiwa saini.

"TPA haijatia saini mkataba na kampuni yoyote. Mkataba uliotiwa saini ni kati ya Serikali ya Tanzania na Dubai kuhusu ushirikiano katika masuala ya bandari, Tehama na mafunzo ya uendelezaji wa bandari. Baada ya hapo kutakuwa na mikataba ya utekelezaji," alisema.

Pia alieleza kuwa katika mikataba kati ya TPA na DP World, mwekezaji huyo atakodishiwa eneo la kufanyia shughuli zake ambazo ataziboresha kwa kuweka mitambo ya kisasa ili meli zishushe mzigo ndani ya siku mbili kutoka wastani wa tisa za sasa. Ni dosari iliyotajwa pia katika ripoti ya CAG ya 2021/22.

**MKATABA WA IGA**

"Kwenye mkataba hakuna sehemu kuna miaka 100, ninafikiri walioleta hilo wana sababu zao na ni upotoshaji wa hali ya juu. Mkataba uliopo una kifungu kinachosema kuna muda wa miezi 12 wa kuridhia na ikipita miezi 12 bila kuridhia maana yake mkataba utakuwa umekwisha," alisema Mbossa.

Alisema mkataba huo unataka kwamba ndani ya miezi 12, pande husika ziwe zimeingia katika majadiliano na kutia saini mkataba na ikishindikana, mkataba utakuwa umekwisha.

"Kipengele cha 23(1) cha mkataba kinaeleza kuwa mkataba utaisha pale mikataba ya utekelezaji itakapoisha," aliongeza.

Alisema iwapo TPA na DP World wakifanikiwa kuingia mikataba baada ya Bunge kuridhia IGA, mikataba itakuwa na muda mahsusi wa kikomo.

"Maana yake ni kwamba muda wa mkataba wa awali utaupata katika mikataba hii inayofuatia," alisema Mbossa.

**UVUNJAJI MKATABA**

Alisema kipengele cha 23 (3) cha mkataba wa IGA kinaruhusu mkataba kuvunjwa au kusitishwa na kinaeleza kuhusu taratibu za kufanya hivyo.

Pia alisema mamlaka hiyo inahusika na bandari za Tanzania Bara pekee kwa kuwa haisimamii bandari za Zanzibar.

"Serikali haijatia saini mkataba wa miaka 100. Serikali haijauiza bandari. Serikali ina malengo mazuri na bandari," alisisitiza.

Kuhusu tuhuma kwa wabunge kupelekwa Dubai, Mbossa alisema watunga sheria hao wamekuwa wakienda sehemu mbalimbali kukagua shughuli za serikali. Kwenda Dubai ni sehemu ya utekelezaji wa jukumu hilo.

**SPIKA AFAFANUA**

Jana asubuhi, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, alisema chombo hicho hakijaridhia azimio kuhusu pendekezo la kuridhia mkataba baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Dubai kwa lengo la kuanzisha ushirikiano wa kiuchumi na kijamii katika uendelezaji wa maendeleo ya bandari nchini tofauti na taarifa zilizotolewa awali na vyombo vya habari.

Vilevile, alitoa wito kwa waandishi wa habari kuzingatia maadili kwa kuhakikisha wanapata taarifa sahihi kutoka katika mamlaka husika kabla ya kutoa taarifa, ili kuepusha kuleta taharuki na usumbufu kwa umma. Chombo cha habari kitakachokwenda kinyume cha angalizo, kuanzia sasa kitachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu za uendeshaji wa shughuli za Bunge hilo.

Akitoa taarifa hiyo jana bungeni, Spika Tulia alisema kwa sasa kamati mbili za Bunge zinazohusika na miundombinu na uwekezaji zinaendelea kupokea maoni ya wadau kupitia njia mbalimbali ikiwamo posta na barua pepe na kuwa linatarajiwa kujadiliwa bungeni Juni 10 mwaka huu.

"Azimio husika kwa sasa bado lipo katika kamati kwa mujibu wa kanuni na mara baada ya kamati kumaliza kazi yake, azimio hilo limepangwa kuingia bungeni Juni 10, 2023 kwa ajili ya mjadala na kupitishwa na Bunge," alifafanua Dk. Tulia.

Alisema kuwa mara baada ya Bunge kupokea azimio hilo, alielekeza lifanyiwe kazi na Kamati ya Miundombinu na Kamati ya Uwekezaji ya Mitaji ya Umma (PIC) ambapo kwa mujibu wa kanuni za Bunge walitakiwa wafanye uchambuzi na kukusanya maoni ya wadau mbalimbali.

Alisema kuwa Juni 5 mwaka huu, kamati ilikaribisha wadau kutoa maoni yao kuhusu azimio hilo na kuhudhuria kikao mahususi cha kupokea maoni katika ofisi za Bunge Juni 6 na sasa kamati ya pamoja inaendelea kupokea maoni kwa wadau ambao hawakufika.

Alisema milango ya Bunge ipo wazi kutoa ufafanuzi wa jambo lolote kutoka kwa waandishi wa habari, hivyo watumie nafasi hizo kupata taarifa zenye uhakika na si kuandika za upotoshaji kwa kuwa chombo chochote kitachotoa taarifa za uongo, Bunge litachukua hatua kwa mujibu wa sheria na taratibu zake.

"...kwa hiyo nitoe wito huo na niseme kwa kweli hili litakuwa ni onyo la mwisho kwa vyombo vya habari vinavyofanya upotoshaji kwa taarifa zinazohusu Bunge," alionya Dk. Tulia.

**ZITTO ALONGA**

Kiongozi wa Chama cha ACT Wazalendo, Zitto Kabwe, hayuko nyuma katika sakata hilo. Ameshauri Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa, aueleze umma usahihi wa kinachoendelea.

"Kwa kuwa kinachokwenda kujadiliwa bungeni ni Azimio la Bunge la Uhusiano kati ya serikali yetu na Serikali ya Dubai, tunawataka wabunge wajadili kwa uwazi kabisa na pale inapowezekana kufanya marekebisho," alisema Zitto katika mkutano wa hadhara wa chama hicho uliofanyika mjini Musoma jana.

Alisema chama hicho kimetafakari kwa kina baada ya kusoma nyaraka mbalimbali zinazohusiana na suala hilo nyeti kwa nchi na kulazimika kutoa kauli hiyo.

Zitto alisema kuna haja wabunge kuhakikisha masuala yanayowatia hofu wananchi yanazingatiwa ikiwamo muda wa mkataba na vipindi vya kufanya marejeo.

"Wabunge wanatakiwa kuzingatia pia suala la maeneo ya makubaliano, suala la kuvunjwa kwa mkataba pale pande mbili zikishindana, umiliki kampuni ya uendeshaji kama itakuwa na hisa sawa kwa sawa kati ya Serikali ya Tanzania na Serikali ya Dubai," alisema.

Alitaja mambo mengine yanayopaswa kuzingatiwa na Bunge ulinzi wa bandari, akisisitiza vyombo vya ulinzi na usalama vya Tanzania pekee ndivyo vitoe ulinzi.

Zitto alisema chama hicho kinawaomba Watanzania kuona umuhimu tujadili masuala hayo kwa misingi ya ukweli bila kuweka hisia ambazo zinagawa taifa.

"Tumefurahishwa na shauku kubwa ambayo wananchi wameonyesha ya kutaka uwazi wa mikataba ya serikali inayoingia kwa niaba ya nchi. ACT Wazalendo tunaamini mijadala ya wazi ni nyenzo muhimu ya kukuza uwajibikaji, demokrasia na maendeleo," alisema.

Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa, Freeman Mbowe, alisema Watanzania wanataka uwekezaji ambao kwa wakati wote utaihakikishia nchi usalama na amani na mataifa mengine ambayo yatatumia bandari.

Alisema ikiwa mwekezaji atakabidhiwa kila kitu katika bandari hiyo, kuna uwezekano wa kuharibu uchumi.

Aliitaka serikali na wabunge kuangalia jambo hilo kwa jicho la kipekee ikiwamo kutoa muda zaidi wa wananchi na wataalamu kutoa maoni yao.

Mbowe alisema hajaona ukomo wa mkataba, jambo ambalo kwake siyo sawa kwa kuwa unaweza kuwa uwekezaji kwa kipindi chote.

"Tunalitaka Bunge likatae kupitisha azimio hili kama serikali haitaliondoa bungeni, lirudi kwa wanachi lipate ufafanuzi. Usiri wa mkataba uondolewe na watu waruhusiwe kulijadili kwa kina. Tumepata nafasi ya kulijadili kwa sababu limevuja mtandaoni," alisema.

Mbunge wa Mvumi, Livingstone Lusinde, alisema jana jijini Dodoma kuwa uamuzi wa serikali kufanya uwekezaji mkubwa katika Bandari ya Dar es Saalam utasaidia wafanyabishara na kuondoa malalamiko ambayo serikali imekuwa ikiyapata muda mrefu.

Alisema watu hawapaswi kuikosoa serikali kutokana na uamuzi wake wa kuikabidhi kampuni binafsi kuendesha bandari kwa kuwa utaleta tija tofauti na ilivyo sasa.

***Imeandikwa na Restuta James (DAR), Julieth Mkireri (MUSOMA) Jenipher Gilla na Paul Mabeja (DODOMA).**

## HABARI KITAIFA

# Mpango aonya bahari kuelemewa na taka ngumu ifikapo mwaka 2050

**Na Romana Mallya**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, amesema endapo hatua madhubuti hazitachukuliwa hivi sasa kudhibiti uchafuzi wa mazingira unaotokana na utupaji wa taka ngumu zikiwamo za plastiki baharini, ifikapo mwaka 2050 bahari itakuwa imeelemewa.

Kauli hiyo inakuja ikiwa ni siku mbili gazeti hili kuripoti changamoto ya taka ngumu kuendelea kutupwa baharini yakiwamo mabomba ya sindano ya hospitali yaliyotumika ambayo huokotwa kwa tani kila mwaka kwenye fukwe na visiwani.

Akizungumza jana jijini Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Bahari Duniani, Dk. Mpango alisema muda mwafaka umefika wa kuweka mikakati na kutafuta njia madhubuti za kulinda na kuhifadhi bahari na rasilimali zake.

"Maelekezo yangu kwa wizara mbalimbali, nianze na ofisi yangu, harakisheni ukamilishaji wa sera ya uchumi wa buluu pamoja na mkakati wa utekelezaji wake. Hakikisheni mnakamilisha maandalizi ya mwongozo wa hifadhi wa mazingira katika uchumi wa buluu. "Wizara ya Uvuvi na Mifugo, simamieni suala la matumizi endelevu na uhifadhi wa rasilimali za bahari, ninatambua mpo katika mchakato wa kupitia na kurekebisha Sheria ya Uvuvi na Sheria ya Uhifadhi wa Bahari na Maeneo Tengefu hili lifanyike haraka na liwe shirikishi.

Makamu wa Rais alisema sheria hizo zimeonesha mapungufu ya kimfumo, kimuundo na kiutendaji katika kusimamia na kutekeleza matamko ya sera ya Taifa ya Uvuvi ya mwaka 2015.

Aliitaka Wizara ya Maliasili na Utalii, ishirikiane na Wizara ya Uvuvi na taasisi za utafiti wa bahari za Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar kufanya utafiti zaidi, ili kuongeza uelewa wa sayansi ya bahari na athari zinazojitokeza. Pia aliwataka watumie mbinu mbalimbali za kuibua namna jamii na taifa zitakavyoweza kunufaika na uchumi wa buluu.

"Hapa niisisitize Wizara ya Fedha na Mipango, ile timu ya wataalam inayoandaa Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2050, ichambue vizuri kwa kina eneo hili ili taifa liweze kufaidika na uchumi wa bahari na fursa ya biashara," alisema.

"Kwa jamii za pwani na visiwani, ni muhimu zihusishwe na zishirikishwe kikamilifu katika ulinzi wa rasilimali za bahari kwa kuwa ndiyo wanufaika na waathirika wa kwanza.Kuhusu wavuvi alisema anafahamu bado kuna baadhi yao wanatumia njia zisizofaa ikiwamo kutumia nyavu zenye matundu madogo zinazovua samaki ambao hawajafikia kuvuliwa na wengine wakitumia mabomu yanayoharibu masalia na wapo wanaotumia sumu.

Alisema mamlaka zinazohusika na uvuvi ziongeze kutoa elimu zaidi kwao ili washiriki katika uhifadhi wa rasilimali za bahari.

Pia alisema ili kufikia malengo waliyojiwekea ni lazima kushirikisha vijana na kulitaka kundi hilo liendelee kuhamasishana na kujiunda na vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na utunzaji wa mazingira na uhifadhi wa bahari.

"Ili kujenga uelewa wa masuala ya bahari na mazingira yake hasa wanafunzi wanaoishi maeneo ya bahari ni vyema nyenzo za ufundishaji na mitaala ya shule za msingi na sekondari zikazingatia masuala hayo.

"Vyombo vya habari na wasanii visaidie jamii kupata uelewa wa kutosha kuhusu bahari na rasilimali zake. Tunawashukuru wadau wa maendeleo kwa kushiriki nasi. "Kama Tanzania itasaidia utaalam na fedha za kutekeleza miradi inayoendana na malengo ya kitaifa tuliyojiwekea kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi na teknolojia ya kisasa zikiwamo za utafiti uvuvi kwenye maji ya kina kirefu.

"Na uhifadhi wa maji ya bahari hususan panapotokea uchafuzi bila shaka tutapiga hatua za kukabiliana na hizi changamoto ambazo tunazizungumza," alisema.

Dk. Mpango alitoa rai kwa jumuiya za maendeleo pamoja na nchi rafiki kutoa fursa za mafunzo kwa wataalam ili wapate uzoefu katika maeneo hayo ya bahari.

Alitaja changamoto zilizopo hivi sasa zinazoathiri uhifadhi wa bahari ni pamoja na mabadiliko ya tabia nchi, uharibifu na upotevu wa viumbe hai, uchafuzi wa mazingira na utupaji wa mifuko ya plastiki.

Kiongozi huyo alisema anafahamu uvuvi wa ovyo umerejea na kuziagiza taasisi zinazohusika kuchukua hatua kukomesha hali hiyo.

Alisema ili kuweza kusimamia na kulinda rasilimali bahari juhudi za pamoja za ndani na kikanda na kimataifa zinahitajika kwa kuwa wanakabiliwa na uwezo mdogo wa teknolojia, upungufu wa rasilimali fedha na rasilimali watu na masuala ya kiutendaji.

Dk. Mpango alikipongeza Kitengo cha Hifadhi za Bahari na Maeneo Tengefu (MPRU) kwa kuzindua tovuti ambayo Meneja wake, Dk. Immaculate Semesi, alisema wanakwenda kujikita katika usimamizi uliojikita kidigitali na kuwaelimisha wananchi umuhimu wa rasilimali za bahari.

Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Abdallah Ulega, alisema wamekubaliana na viongozi wa dini kusaidia kutoa elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kutunza bahari na kujiepusha na vitendo vinavyoharibu rasilimali hiyo.

# Wazazi wajijazia kadi kliniki watoto bila kufika vituo afya

**Na Christina Mwakangale**

KINAMAMA wenye watoto walio katika umri wa kuhudhuria kliniki (chini ya miaka mitano), wamebainika kujijazia kadi za kliniki za watoto wao badala ya watoa huduma za afya.

Ni dosari inayotajwa kuathiri maendeleo ya ukuaji wa mtoto na kuchangia kuwa na udumavu.

Hayo yamebainishwa na watoa huduma za afya ya mama na mtoto kutoka Hospitali ya Teule ya Wilaya Ifisi, iliyoko Mji wa Mbalizi, nje kidogo ya Jiji la Mbeya. Wadau hao wa afya walikuwa wanatoa huduma ya kliniki na chanjo kwa kinamama waliofika hospitalini huko na watoto wao kwa ajili ya kupatiwa huduma kiafya.

Ofisa Muuguzi Msaidizi wa hospitali hiyo, Herrieth Mwasenga, alisema walibaini hilo kupitia kliniki. Ni vitendo vinavyoathiri ukuaji na maenedeleo ya mtoto kwa kuwa ni vigumu kubaini iwapo mtoto ana tatizo kiafya.

"Kuna hasara kubwa mama asipomleta mtoto kliniki, kwa sababu anapokuja kliniki anapata elimu kuhusu watoto, kwamba mtoto malezi yake yawe ya aina gani. "Katika kliniki, kuna elimu, kuna ngazi ya mtoto mmoja hadi mwingine, uzazi wa mpango, yaani unapishanisha mtoto huyu na mwingine baada ya miaka kadhaa," alisema muuguzi huyo.

Leah Mwakasungula, muuguzi kutoka hospitali hiyo, alisema tatizo la kinamama kujijazia kadi za kliniki limekithiri vijijini Mbeya. Wanaendelea kutoa elimu. Wameweka utaratibu mara moja kwa wiki, siku ya Alhamisi ambayo pia ni maalum kwa ajili ya kutoa chanjo.

Sara Kilala, mzazi ambaye pia ni mkazi wa ZZK, Mbalizi, alisema elimu kuhusu malezi ya watoto ni muhimu. Anakiri baadhi ya kinamama wanajaza kadi za kliniki za watoto wao pasi na kuhudhuria kliniki. Ni hatua inayokinzana na uhalisia wa makuzi ya mtoto.

"Mtoto wangu alipoumwa nikaambiwa namna ya kuchanganya lishe, ndio maana kila mwezi unaambiwa ufike kliniki. Utakuta mwingine unamshauri aende kliniki, anakujibu 'kwani kuandika tu katika kadi kuna shida gani?'

"Anajijazijia tu mwenyewe, ila madhara hatoyaona hapohapo kwa sababu mimi ninayeenda kliniki ninapata elimu kuhusu umri na uhalisia wa mtoto.

"Mfano, mtu akijaza kadi mwenyewe atakadiria tu ile grafu, kwamba isome kwenda juu, anadanganya, ila siku mtoto akiumwa wanaangalia kadi na kupewa dawa kulingana na uzito wa mtoto, kumbe uzito halisi ni mdogo, ila kadi amejaza uongo, mtoto atakuwa haponi," alionya Sara. Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Sauti ya Mama Afrika (SAMAFO), Tabitha Bugali, alisema taasisi hiyo ilifika hospitalini huko ili kutoa elimu ya lishe na afya ya uzazi kwa kushirikiana na Kituo cha Hope, maarufu Kwa Mchungaji Lena, kinachojihusisha na masuala ya watoto na wenye mahitaji maalum. Ni maandalizi ya kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mtoto wa Afrika Juni 16.

Kuruthum Mbekae, Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambaye pia ni Mratibu wa Dawati la Watoto na Wanawake, alisema kuelekea maadhimisho hayo, kunatolewa mafunzo ya malezi ili kumlinda mtoto dhidi ya ukatili.

Musa Simyenga, Mratibu wa Kituo cha Hope, alisema jamii isiwe na ukimya katika vitendo vya ukatili dhidi ya watoto, akiwataka wazazi waache kumalizana nyumbani pindi kunapojitokeza matukio ya ukatili.


AGENZIA ITALIANA PER LA COOPERAZIONE ALLO SVILUPPO | Servizio di pace LVIA | DIVERSE FOOD SYSTEM

**MOTOR VEHICLE AND MOTOR BIKE(s)**

**AID012590/08/9/2022/TZ/06**

LVIA Tanzania intends to award a supply contract for Purchase of Motor Vehicle and Motor Bikes in Dodoma with financial assistance from the project name DIVERSE FOOD SYSTEM, improving nutrition by supporting a diversified and sustainable food system. AID 012590/08/9

The tender dossier is available from LVIA head office located in Dodoma Area D Sengia street or via the following link

**https://drive.google.com/file/d/1kOaET280-NIg95dczO8VVvizNTGObsyJ/view or using Website www.zabuni.co.tz**

The deadline for submission of tenders is **30/06/2023**

Possible additional information or clarifications/questions shall be requested via email address **cr.tanzania@lvia.it** or at the office with the Address above.



Victoria FINANCE

Victoria Finance Plc
5th Floor, Sky Tower Building Kijitonyama
New Bagamoyo Road
P.O. Box 12102, Dar es Salaam - Tanzania

Telephone +255 22 277 4577
Fax: +255 22 277 4559
Email info@victoriafinance.co.tz
Website www.victoriafinance.co.tz

**TANGAZO LA MINADA YA HADHARA**

VICTORIA FINANCE PLC INAPENDA KUUTANGAZIA UMMA YA KWAMBA KWA IDHINI ITAKAYOTOA KWA KAMPUNI TOFAUTI ZA UDALALI INATARAJIA KUUZA KWA MNADA WA HADHARA DHAMANA ZA WADAIWA SUGU KAMA IFUATAVYO;

| S\NO | CREDITOR'S NAME | BAIL | TYPE AND PART OF THE GUARANTEE | AUCTIONEER | DATE |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | PATRICIA ISAACK MANYAMA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – MBAGALA | JODAC PROFESSIONALS | 24-06-2023 |
| 2 | ADINI HODLAM MSANYA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – KILOSA MOROGORO | J & J RECOVERIES | 24-06-2023 |
| 3 | PHILIPO RAPHAEL KOMBA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI – KILOSA MOROGORO | J & J RECOVERIES | 24-06-.2023 |
| 4 | MICHAELY EDWARD MICHAELY | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – DAKAWA MOROGORO | J & J RECOVERIES | 01-07-2023 |
| 5 | FELIX KIMARO. DAUDI | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – UBUNGO MAZIWA | JOFORTE AUCTION MART | 24-06-2023 |
| 6 | SAMWELI KAPULWA KOTIPE | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – DAKAWA MOROGORO | J & J RECOVERIES | 24-06-2023 |
| 7 | RESPIQUIS MUTTA | NYUMBA | LESENI YA MAKAZI - KITUNDA | LEHALEL GROUP OF COMPANY LIMITED | 24-06-.2023 |
| 8 | PAULINA A. MWANGA | NYUMBA | MKATABA WA MAUZIANO – MALAMBA MAWILI | JOFORTE AUCTION MART | 24-06-2023 |

Minada yote itafanyika mahali husika katika muda na siku ambayo itatangazwa kupitia katika vipeperushi na magari ya matangazo kutokana na idhini itayotoka kutoka katika vyombo husika vya Serikali.

**MASHARTI YA MNADA;**

- Asilimia 25% ya bei iliyofikia italipwa papo hapo na asilimia 75% iliyosalia ilipwe ndani ya siku kumi na nne. (14). Kwa kushindwa kufanya hivyo itapelekea mnada kurudiwa tena na pesa zilizolipwa kutokurudishwa.
- Gharama za kumuhamisha mmiliki na kubadili umiliki ni juu ya mnunuzi.
- Dhamana itauzwa Kama ilivyo.



Katibu Tawala wa Wilaya ya Kahama, Timothy Ndanya (wa tatu kulia), akipata maelezo wakati wa mafunzo ya siku moja kuhusu kilimo bora kwa wakulima wa wilaya hiyo, yaliyoandaliwa na Taasisi ya EFTA mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Mkurugenzi Mtendaji wa EFTA, Nicomed Bohay. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Majahazi yanaswa na madumu 925 ya mafuta ya magendo

**Na Halfani Chusi**

JESHI la Polisi Kikosi cha Wanamaji, kimewakamata watu wanane na majahazi mawili yenye shehena ya madumu 925 ya mafuta ya kupikia yaliyoingizwa bila kibali kutokea Zanzibar.

Taarifa iliyotolewa jana kwa umma na Kamanda wa Polisi Kikosi cha Wanamaji Tanzania, Kamishna Msaidizi (ACP) Moshi Sokolo, ilisema watuhumiwa hao walikamatwa kwenye operesheni iliyofanyika Bahari ya Hindi, juzi maeneo ya Kunduchi, Kinondoni mkoani Dar es Salaam.

Alisema katika operesheni hiyo, Kikosi Kazi cha Polisi Wanamaji Dar es Salaam, kikitumia boti, juzi majira ya saa 9:00 usiku, kilikamata majahazi mawili yakiwa na shehena ya mafuta ya kupikia kwenye madumu 295 ya lita 20 kila moja yakitokea Zanzibar kwenda bandari bubu ya Kunduchi.

Kamanda Sokolo alisema jahazi la kwanza lilitambulika kwa jina la MV NI CHACHE SANA lenye namba za usajili Z 2575, lilikuwa linaongozwa na Nahodha Hamad Mzee Idd (36), Mkazi wa Mwera, Zanzibar, akiwa na wenzake wanne. Alisema katika jahazi hilo kulikuwa na madumu 573. Alisema jahazi la pili, lilitambulika kwa jina SV NASI HULA, lenye namba za usajili Z 3164 likiwa na madumu 352 lililokuwa likiongozwa na Nahodha Ramadhan Juma Khamis (27), mkazi wa Zanzibar kwa Seif, akiwa na wenzake wawili.

Sokolo alisema katika uchunguzi wa awali, walibaini kuwa watuhumiwa hao hawakuwa na nyaraka zinazothibitisha uhalali wa umiliki wa mzigo huo pamoja na nyaraka za usafirishaji.

Alitoa onyo kwa wafanyabiashara wasio waadilifu kuacha kusafirisha mzigo kwa njia ya bahari bila kuwa na nyaraka huku akisisitiza hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya yeyote atakayebainika.

# Ajali tatu, vifo saba, majeruhi 24 wiki moja

**Na Mwandishi Wetu**

NI wiki ya mfululizo wa ajali katika barabara ya Morogoro - Iringa baada ya watu wengine wawili kufariki dunia na mwingine kujeruhiwa katika ajali ya gari aina ya Toyota Harier kugongana na Mitsubishi Fuso katika eneo la Melela Mangae.

Ajali hiyo ni ya tatu kutokea katika barabara hiyo, ya kwanza ilitokea eneo la Iyovi ambapo Juni 5, mwaka huu. Watu watano walipoteza maisha na 20 kujeruhiwa baada ya Toyota Coaster ya kukodi kugongana na lori. Nyingine imetokea jana ndani ya hifadhi ya Taifa ya Mikumi ikihusisha Toyota Noah na Fuso na watu wanane walijeruhiwa vibaya.

Kwa mujibu wa mashuhuda wa ajali hiyo iliyohusha gari Harrier na Fuso katika eneo la Melela Mangae, watu wawili waliopoteza maisha na mwingine kujeruhiwa. Wote walikuwa kwenye Harrier.

Baadhi ya mashuhuda, Jabir Abdalah na Adilinia Juma, wakazi wa Melela Mangae, kwa nyakati tofauti walisema ajali hiyo ilitokea majira ya usiku na miili ya marehemu na majeruhi walipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro.

"Nilisikia kishindo kikubwa na baada ya kutoka tukakuta magari haya yamegongana na gari ndogo kuharibika vibaya. Ndani ya gari dogo walikuwa watu watatu na wale waliokuwa mbele ndio walikufa kwenye ajali na yule wa nyuma akajeruhiwa," alisema Juma.

Mashuhuda hao walibainisha kuwa miili ya waliopoteza maisha na majeruhi ilichukuliwa usiku na polisi waliofika eneo la tukio na kwamba kwenye Fuso hakuna mtu yeyote aliyejeruhiwa.

Nipashe ilimtafuta Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Kamishna Msaidizi (ACP) Alex Mkama, lakini hakupatikana kuzungumzia matukio haya na baadaye alipopokea simu, alisema yuko kwenye kikao.

# Miswada Tume Mipango, Usalama wa Taifa yapita

**Na Jenifer Gilla,** DODOMA

BUNGE limepitisha miswada mitatu ya sheria ikiwamo wa Marekebisho ya Sheria ya Tume ya Mipango chini ya ofisi ya Rais itakayokuwa na jukumu la kubuni, kupanga, kuratibu na kusimamia mipango ya maendeleo ili kuwa na mfumo jumuishi wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa vipaumbele vya taifa.

Akiwasilisha muswada huo bungeni jana, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, alisema kupitia muswada huo pia kutakuwa na utaratibu wa kupanga pamoja mipango ya kisekta hususan sekta zenye majukumu yanayotegemeana.

Pia alisema kutakuwa na mfumo wa kisheria na chombo mahususi cha kusimamia uandaaji, utekelezaji wa mipango ya maendeleo, utafiti na kuishauri serikali kuhusu vipaumbele vya maendeleo ya taifa, majukumu ambayo kwa sasa yanatekelezwa na Wizara ya Fedha na Mipango.

Aidha, bunge limepitisha muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Idara ya Usalama wa Taifa ya mwaka 2023, ili kuifanya idara hiyo katika kutekeleza majukumu yake kuwajibika moja kwa moja kwa Rais.

Simbachawene alisema kifungu cha nne ili kuipa idara hadhi ya chombo cha ulinzi na usalama chini ya Rais.

Pia alisema mswada huo utafanyia marekebisho kifungu namba tano, ili kuyapa nguvu ya kisheria majukumu ya msingi na muhimu ya usalama ambayo kwa sasa yanatekelezwa na idara lakini hayatambuliwi na sheria.

"Majukumu hayo ni pamoja na ulinzi binafsi wa viongozi wa kitaifa na kimataifa, ulinzi wa vituo muhimu,mamlaka ya upekuzi wa kiusalama wa viongozi na udhibiti wa matishio ya kiusalama dhidi ya Jamhuri wa Muungano," alisema Simbachawene.

Vilevile Muswada wa Urekebu wa Sheria Mbalimbali wa mwaka 2023, utakaofanyiwa marekebisho sheria nane ikiwamo Sheria ya Uanzishwaji wa Mashirika Binafsi sura ya 119 na Sheria ya Usimamizi wa Tozo na Ushuru wa Bidhaa sura 147.

Sheria nyingine zitakazofanyiwa marekebisho kwa mujibu wa Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro, ni Sheria ya Kodi na Mapato sura ya 332, Sheria ya Tafsiri ya Sheria sura ya kwanza, Sheria ya Urekebu wa Sheria sura ya 4, Sheria ya Hifadhi za Jamii sura ya 135, Sheria ya Mamlaka ya Mapato sura ya 399 na Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi sura ya 363.

MAONI YA WABUNGE

Mbunge wa Bukene, Selemani Zedi, alipongeza maboresho ya Sheria ya Usalama wa Taifa iliyopo yenye lengo la kuweka muundo wa kisasa wa kufanya ufanisi kwa idara hiyo, ikiwamo ibara ya pili ambayo inampa Rais jukumu la usalama wa taifa badala ya waziri.

Alisema badiliko la kimuundo ni jambo la kuunga mkono kutokana na umuhimu wa chombo hicho kwa taifa na pia itarudisha hadhi ya chombo hicho.

"Kwa hiyo Mheshimiwa spika, ninawaomba sana waheshimiwa wabunge tukubali marekebisho ya sheria hii ya idara ya usalama wa taifa hasa kifungu hiki cha ibara ya pili ambayo kimsingi inakabidhi jukumu hili ambalo ni muhimu sasa lisimamiwe moja kwa moja na mheshimiwa rais mwenyewe," alisema.

Aidha, alipongeza marekebisho ya ibara ya 15 ya sheria hiyo ambayo sasa yanaipa idara hiyo jukumu la kukusanya taarifa za kiitelijensia kwa ajili ya kufanya ulinzi kwa maeneo muhimu ya kiuchumi kwa kuwa kuna baadhi ya maeneo yakifanyiwa hujuma yanasababisha tatizo kubwa la kiuchumi hasa kipindi hiki ambacho nchi inafanya uwekezaji mkubwa.

Mbunge wa Kiteto, Edward Ole Lekaita, alisema kupitia Sheria ya Mpango wa Taifa anategemea kuona mipango ya maendeleo ya taifa kuwa ya muda mrefu itakayoongoza taifa na itakayoratibu mipango ya wizara nyingine na kutoa ajira za kimaendeleo kwa taifa hilo.

Alisema muswada huo utairudisha tume ya mpango wa taifa ikiwa na sura na majukumu mapya kutoka 11 yaliyokuwapo kabla haijafutwa na sasa yapo 16 na matgemeo yake kuwa tume hiyo itafanya kazi kwa ufanisi zaidi ili kuiletea nchi maendeleo.

"Na utafiti duniani unaonyesha nchi zinazofanya vizuri kwa mfano Ghana, Indonesia, Afrika Kusini na India, zote zina tume hii na mwenyekiti wa tume ni Mheshimiwa Rais," alisema.

# TANGAZO

TEMBO NICKEL

# VACANCIES

## PROCUREMENT LEAD-KABANGA

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit **a Procurement Lead** to join the Tembo Nickel Project Team. This role is based at **Kabanga site.** The successful candidate will be accountable in managing Demand Planning, Procurement, and Logistics of various materials required for Tembo Nickel Project. The successful candidate will play a key role in liaising with the Mining Commission and ensuring compliance with Local Content regulations. This role will report to the **Procurement Manager** and will work on **6/3 roster.**

**Duties and Responsibilities**
- Support of field construction teams related to complex equipment needs and tight project schedules.
- In conjunction with other stakeholders, define business rules relating to demand management and to effectively implement these for improved supply and cost.
- To drive the demand planning process at the Mine and Refinery sites to ensure that exceptions in demand are communicated effectively and that the required decisions are made to manage the change in demand with minimal impact on the Construction Schedules.
- To monitor suppliers' technical quality, delivery and financial performance.
- To identify and implement opportunities for reduction in lead time and inventory for total cost reduction in Supply Chain of the Mine.
- All items are procured and expedited effectively to reach the mine on time Work with Community Relations to assess and develop Local Enterprises.
- To take part in identifying cost saving opportunities and work with suppliers to reduce material costs.
- To take place in tender evaluation committee as a commercial member.
- To effectively implement contactors scorecard review meetings.

**Required Qualifications**
- Bachelor's degree in supply chain and Logistics management
- PSPTB certification is a MUST.

**Experience Requirements:**
- 5 Years of work experience in Supply Chain and Logistics Management with at least 2 years in demand management/Inventory management role

**Skills and Knowledge**
- Strong Analytical Skills
- Excellent interpersonal Skills
- Excellent working and demonstrated knowledge of ERP/PRONTO systems and MRP.
- Business acumen and excellent work ethics,

## SAFETY OFFICERS-KABANGA (3)

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to **recruit Safety Officers** to join the Tembo Nickel Project Team. This role is based at **Kabanga site.** The safety officers will work to ensure provision of service and support to employees and supervisors in respective departments across Tembo Nickel Project regarding employees' Health and Safety in the workplace. Supporting TNCL operations to ensure that safety objectives are aligned with the business plans and that all safety programs are in accordance with organization standards and legislative requirements.

**Duties and Responsibilities**
- Lead and influence change whilst developing a positive safety culture.
- Provide support and guidance to Safety Representatives.
- Conduct on job coaching and training to employees on Standard Operating Procedures (SOPs) and safe work practices.
- Conduct scheduled weekly and monthly Safety meetings.
- Detail knowledge of establishing and implementing ISO 45001:2018 management system.
- Participate in the review of Standard Operating Procedures.
- Conduct workplace inspections and audits as required.
- Assist in incident and accident investigations.
- Monitor and follow up on incident investigation recommendations to ensure actions are completed and implemented.
- Ensure compliance with relevant Tanzanian Occupational Health and Safety regulations.
- Correct and report safety hazards when observed.
- Assisting with the facilitation of formal risk assessments.
- Understanding of related department activities and managing their impact on the safety programs

**Qualifications**
- Tertiary qualification in health and safety management or equivalent from a Tanzanian or internationally recognized institution.
- ISO 45001:2018 OHS Management system certification.
- Formal Training Qualification in Risk Management, Accident Investigations, and Occupational Health and Safety.
- Tanzania OSHA – NOSCH I & II.
- 3 - 4 years' experience in Safety Practice in Mining, Processing, or Maintenance disciplines. Construction experience is an added advantage.
- A Valid Tanzania Driving License.

**Skills and Knowledge**
- Sound knowledge of Legislative Requirements within Mining - OSHA, Mining Act, Explosives Act, Mines Health & Safety Act, Mining Regulations,
- Hazard identification and Risk assessment
- Incident and Accident investigating

## ERT OFFICER-KABANGA

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit **an Emergence Response Team officer** to join the Tembo Nickel Project Team. This role is based at **Kabanga site.** The ERT Officer ensures provision of emergency response leadership, leads the Emergency Response Team (ERT) to the rescue event, and provide basic training related to evacuation plan, emergency exits, and ERT training.
- Ensure total compliance/adherence to all safety, occupational health, and safety policies and procedures as well as policies and procedures, and guidelines.
- Follow work schedules to maximize efficiency, taking into consideration roles and responsibilities in cooperation with other team members.
- Responsible for incidents, including natural disasters (Fire and water rescue), and assess the situation to determine the level of response required and assist with any other accident/incident onsite and offsite.
- Identify all unsafe acts, situations, and hazards within ERT training and real emergency.
- Ensure all fire equipment inspection and rescue, ensure fire extinguishers are properly inspected, and update records on the register.
- Contribute and support the scheduled ERT training.
- Conduct training of Emergence team members
- Carry out an inspection of the airstrip and ensure the landing and take-off happen according to the timetable.
- Provide basic training related to Evacuation Plans, emergency exits, and PPEs to employees, contractors, and suppliers.
- Act as duty officer as part of a 24-hour duty system, responding to emergency situations as they arise.
- Perform related duties as may be assigned from time to time by supervisors or Managers.

**QUALIFICATIONS**
- Certificate/ in Emergency Management
- NOSCH I and II - OSHA Tanzania
- Industry Fire Training
- Rescue Certificates on BG4, Fire Rescue, Rope Rescue, Hazmat, SCBA, and Vehicle extrication
- Evidence in heat tolerance and workload training.
- Mine Health & Safety Act awareness.
- A Valid Tanzania Driving License.

**SKILLS, KNOWLEDGE, AND EXPERIENCE**
- 4-5 experience in Mining operations, Processing, and Construction
- Experience in attending Aviation Activities
- Good communication skills.
- Experience in facilitating training courses, BG4, BA open circuit, use of Fire equipment, lifter bags, and vehicle extrication.

## SAFETY ADMINISTRATOR-KABANGA

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit **Safety Administrator** to join the Tembo Nickel Project Team. This role is based at Kabanga Site. The Safety Administrator will be responsible in providing general administration and support to the health and safety team, including but not limited to the overall operations of the OHS department.

**Duties and Responsibilities**
- Execute developed environmental management plans, programs, and strategies on site.
- Plan environmental projects and provide reports on status and outcomes.
- Prepare written reports as required, briefs for projects and or services, strategies, policies, and management plans.
- Assist in the coordination of field personnel to ensure works are completed to specified standards.
- Provide technical input into the development of environmental policies, guidelines, and procedures for Tembo Nickel.
- Conduct the environmental incident reporting & incident investigation program.
- Oversee contractors and consultants as per the company's standard operating procedures.
- Ensure monitoring programs of air quality, water quality, noise & vibration, meteorological, soil and biodiversity are maintained and undertaken in a timely and cost-effective manner.
- Facilitate the dissemination of information and training of environmental management aspects for all employees.
- Provide input to Environmental Lead into the development of environmental quality standards, guidelines, objectives, policies, procedures and/or legislation.
- Carryout inspections, conduct investigations, resolve conflict, and take appropriate action.

**Qualifications and Competencies**
- Bachelor's degree in environmental science or Environmental Engineering or related discipline. Master's degree in science/Environment is an added advantage.
- Minimum of 3 years working experience in environmental management role in a large-scale operation preferably in the mining and extractive industry. Experience in the application of EHS management systems.
- Knowledge on ISO 14001 EMS implementation process
- Good understanding of Audit/EMS management systems
- Knowledge of NEMC registrations for Audit and EIA

Tembo Nickel offers a competitive remuneration package and **ONLY** shortlisted candidates will be contacted.

**How to Apply**
Applicants are invited to send their resumes indicating the role title in the subject via email **jobs@tembonickel.com**
**Application closing date is 16th June,2023**
***Note:*** *We are committed to provide equal employment opportunities based on merits and we do not charge candidates any fees in the whole recruitment process.*

**Women are strongly encouraged to apply.**

**For and behalf of Tembo Nickel, Kabanga Nickel Project.**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wizi vibao vya anwani za makazi ni kurudisha nyuma maendeleo

**WIMBI** la wizi wa vibao vya anwani za makadhi katika baadhi ya mikoa unaofanywa na watu wanaodaiwa kwenda kuviuza kama vyuma chakavu ni kurudisha nyuma maendeleo ya nchi.

Hivi karibuni ilibainika katika Mkoa wa Mbeya kuwapo watu wanaoiba vibao hivyo ambavyo vimewekwa ili kutambulisha mitaa na kurahisisha wageni kufika mitaa husika kwa urahisi.

Katika kudhibiti wizi huo, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, ameagiza watendaji wa kata, vijiji na maofisa tarafa kufanya msako na kuwakamata wananchi wote wanaohusika kuiba vibao hivyo vya anwani za makazi vilivyowekwa kwenye mitaa mbalimbali mkoani humo.

Agizo hilo alilitoa wakati alipopokea ripoti ya uchambuzi ya Sensa ya Watu na Makazi kwa mkoa wake ambayo ilihusisha viongozi mbalimbali wa mkoa huo na timu ya wataalam waliohusika kwenye mchakato wa kukamilisha kazi hiyo.

Alibaini kuwapo kwa baadhi ya maeneo vibao kung'olewa na watu wasiokuwa waadilifu na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu na wengine kuweka katika ofisi zao.

"Tayari watu wameanza kung'oa vibao kwenye mitaa yao na kwenda kuviuza kama vyuma chakavu ili wajipatie pesa sasa naagiza watendaji wote na maofisa tarafa kushughulikia suala hili, najua mnawafahamu na mtawakamata nendeni mkalitekeleze hili ili liwe fundisho kwa wengine kwa sababu wanatuhujumu."

Kwa kweli kitendo hicho kinasikitisha na kinakwamisha jitihada za serikali za kurahisisha mawasiliano kwa kuwa kuondolewa kwa vibao hivyo kutasababisha wageni kushindwa kufika maeneo wanayokusudia.

Katika miji mingi kwenye nchi zilizoendelea na baadhi ya zinazoendelea, imekuwa rahisi kwa mgeni anapoelekezwa kufika kwa urahisi kutokana na kuwapo kwa anwani za makazi na vibao vinavyoongoza kwenye mitaa hiyo.

Wageni kutoka nchi za mbali wanapotembelea nchi za kigeni hupata urahisi wa kufika mahali wanapokwenda kutokana na kuwapo na mipango miji mizuri na yenye anwani za makazi.

Mgeni anaweza kufika sehemu husika kwa kuangalia tu ramani, bila kumuuliza mtu yeyote kumuelekeza.

Serikali inajitahidi kuifanya nchi kuwa kwenye mipango miji mizuri kwa kuweka anwani za makazi ili kuwarahisishia wageni.

Kwa mujibu wa sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 kwa Mkoa wa Mbeya, idadi ya watu ni 2,343,754 ikilinganishwa na mwaka 2012 iliyokuwa 1,708,548 sawa na ongezeko la 635,206.

Ongezeko hilo ni sawa na asilimia 3.2 ambayo sasa mkoa utaweka mipango madhubuti kwa ajili ya kukamilisha shughuli za miradi ya maendeleo.

Takwimu hizo zitasaidia kuongeza uwazi ili wawe na uelewa wa matumizi ya matokeo ya sensa kwa ajili ya kutoa michango yao kwa ajili ya maendeleo ya taifa na kushauri namna bora ya kuyapima.

Mstahiki Meya wa Halmshauri ya Jiji la Mbeya, amehakikisha jiji hilo kuandaa mipango kabambe kwa ajili ya kuwasaidia wananchi kwa kuzingatia idadi ya watu.

Pia, wananchi wameombwa kuishauri serikali namna bora ya kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo na kusisitiza kutoa ushirikiano ili ikamilike kwa wakati.

Katika hili wananchi lazima wakumbuke kuwa maendeleo yoyote yanayofanywa ni kwa ajili yao, kuhujumu maendeleo hayo ni sasa na kujihujumu wenyewe.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ripoti ya utafiti huu ifanyiwe kazi kulinda lishe na afya za wanafunzi

Na Sabato Kasika

**TAASISI** ya Chakula na Lishe Tanzania, kwa kushirikiana na Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Malaria, zimetoa ripoti ya utafiti wa kutathmini kiwango cha maambukizi ya malaria na utapiamlo miongoni mwa wanafunzi na kuibuka na matokeo yanayoonyesha afya zao si salama.

Utafiti huo wa mwaka 2021, ulihusisha mikoa 26 ya Tanzania bara, shule 650 na wanafunzi 64,465 ambao ripoti yake ilitolewa mnamo Machi mwaka huu, ikielezea hali ya lishe ya wanafunzi wa shule za msingi nchini zilivyo.

Utafiti huo kimsingi, ulilenga kutathmini kiwango cha maambukizi ya malaria na utapiamlo miongoni mwa wanafunzi, ambao katika viashiria vya lishe, utafiti ukabaini kwamba wanafunzi waliopo katika shule za msingi bado wana changamoto nyingi za lishe zinazowakabili.

Mbali na hayo, watafiti hao pia wanaeleza kubaini wanafunzi wengi bado wana lishe duni, uzito uliopungua, uzito uliokithiri na upungufu wa damu kwa kiwango kikubwa.

Aidha wanataja shule nyingi zimezungukwa na maduka na vibanda vya wauzaji wadogo wadogo wa vyakula, lakini bahati mbaya ni kwamba, utafiti huo ulibaini kuwapo kwa vyakula ambavyo si rafiki kwa afya za wanafunzi.

Kwa matokeo hayo, ninadhani ingekuwa ni vyema matokeo ya utafiti huo yakafanyiwa kazi haraka, ili kulinda afya za watoto wa shule, kwani siyo siri, shule nyingi zimezungukwa na maduka na vibanda hivyo.

**Ninaunga mkono juhudi hizo za serikali na wadau wake, hasa kutokana na ukweli kwamba lishe duni inasababisha madhara ya udumavu, upungufu wa damu, upungufu wa vitamini A, utapiamlo mkali, kupungua uzito au uzito uliokithiri.**

Pia, si maduka na vibanda pekee, kwani wapo baadhi ya mamalishe wanaokaanga mihogo na viazi katika maeneo ya shule na kuwauzia wanafunzi. Sidhani kama wote wanazingatia kanuni sahihi za afya kwa ujumla.

Kwa kuwa serikali imekuwa ikitoa mafunzo katika maeneo mbalimbali ikiwamo shuleni, ili kukabiliana na tatizo hilo la lishe duni, ninadhani pia ipo haja ya kutumia utafiti huo, ili kusaidia wanafunzi kuwa salama.

Mafunzo hayo yamekuwa yakitolewa kwa walimu wakuu wa shule za msingi na sekondari, kwa lengo la kuwajengea uelewa kuhusu elimu ya lishe bora katika shule zao.

Kwa kuwa mafunzo hayo yanalenga kusaidia walimu na wanafunzi kuwa na uelewa katika umuhimu wa lishe na kuwa mabalozi wazuri katika jamii, ninadhani kupitia ripoti hiyo, maeneo ya shule yanatakiwa kuuzwa vyakula ambavyo ni rafiki kwa afya za wanafunzi.

Ninaunga mkono juhudi hizo za serikali na wadau wake, hasa kutokana na ukweli kwamba lishe duni inasababisha madhara ya udumavu, upungufu wa damu, upungufu wa vitamini A, utapiamlo mkali, kupungua uzito au uzito uliokithiri.

Vilevile inaelezwa kuwa madhara ya lishe kwa wanafunzi ni pamoja na kiwango hafifu cha ufaulu, kutumia muda mrefu kuwafundisha, watoto kushindwa kuhudhuria masomo kila siku na magonjwa.

Hivyo basi, uamuzi huo wa kutoa mafunzo shuleni ni vyema uendelee kusambaa katika shule zote nchini, kwani suala la lishe bora lina changamoto kubwa inayohitaji ufumbuzi wa haraka.

## HABARI KITAIFA



Makamu wa Rais wa kiwanda cha uzalishaji wa pikipiki aina ya TVS cha India, Rahul Nayak (kushoto), akizungumza na wafanyakazi wenzake, jijini Dar es Salaam jana, baada ya ziara yake ya kuwatembelea mawakala wa usambazaji na uuzaji wa bidhaa hiyo. **PICHA: HALFANI CHUSI**

# TRA: Tutafuata misingi, haki kuwachukulia hatua wakwepakodi

**Na Christina Mwakangale**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA), imesema kwa nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania, mkwepa kodi haoni aibu hata akitangazwa hadharani, mamlaka hiyo haitasita kufuata misingi tisa ya kikodi, ikiwamo kufanya ukaguzi wa risiti kwenye biashara yoyote.

Imesema TRA inaendelea kutoa elimu kwa wananchi na wadau wengine ili kubainisha umuhimu wa kodi, haki na wajibu wa mlipakodi na kuwachukulia hatua za kisheria wakwepaji kodi.

Ofisa Mkuu wa Usimamizi wa Kodi wa TRA, Hamad Mterry, aliyasema hayo juzi, jijini Dar es Salaam, wakati akiwasilisha elimu ya mlipakodi kwa wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari Dar es Salaam (DCPC).

Alisema kulipa kodi inayokusanywa na serikali kuu kupitia mamlaka iliyopo kisheria, ni lazima bila kujali mlipakodi amepata elimu kuhusu kodi au la, ingawa mamlaka hiyo haijawahi kusita kuuelimisha umma.

"Duniani huwezi kukwepa vitu viwili; kodi na kifo. Hakuna haki bila wajibu. Unakula kila siku utalipia tu kodi, haikwepeki. Kodi ni taaluma aihitaji kada moja, mfanyabiashara, mchumi, mhasibu, mwalimu. Kwenye kodi hakuna usawa (equality) kuna uwiano (equity) kulipa kodi kadri ya unachopata.

"Anayepata kikubwa alipe kikubwa, anayepata kidogo alipe kidogo. Kuanzia sasa badala ya kutumia utambulisho wa vitambulisho, unatumika utambulisho wa TIN namba na namba hii inatakiwa kutundikwa au kuwekwa kwenye biashara yako ikiwa ni cheti halisi na si kopi," alisema Mterry.

Alisema mlipakodi ana haki ya kupinga kodi iliyokokotolewa, ikiwamo kukata rufani na kufika kwenye ngazi za kimahakama katika mahakama zinazoshughulikia kodi, huku akisema wajibu wa mlipakodi pia ni kujiandikisha kwenye mifumo ya kikodi ikiwamo TIN namba na EFDs.

"Ukiona tunaenda Kariakoo tunakagua risiti ni mbinu za kukagua, ili tujue, tusipokagua tutaulizwa. Suala hili halikwepeki, tukiacha tutakosa kodi. Ukikwepa kodi, kwa nchi za wenzetu na wakitangazwa kwenye vyombo vya habari ni aibu, hapa kwetu mtu mkwepaji na haoni aibu," alisema Mterry.

Awali, Mkurugenzi wa Elimu na Huduma kwa Mlipakodi TRA, Richard Kayombo, alisema kasi ya ulipaji kodi imeongezeka na hali hiyo inaashiria kufanikiwa kufikia lengo la kukusanya Sh. trilioni 23.1 kwa mwaka wa fedha 2022/23.

Kayombo alisema elimu wanayoitoa kwa makundi mbalimbali pamoja na waandishi wa habari ambao ni nguzo muhimu katika kutoa elimu ya ulipaji wa kodi, kumeleta mabadiliko ya mamlaka hiyo kukusanya kodi.

Alisema kupitia mafunzo hayo jamii imepata elimu kuhusu faida za kulipa kodi, hali inayowasaidia TRA kukusanya mapato kwa uhakika na wakati.

"Siku zote kodi sio kitu kinachopendwa na binadamu, kunahitajika elimu na wakati mwingine sheria itumike mtu alipe kodi. Ukijiimarisha na kodi utakuwa huru, utaepuka matakwa ya mtu anayekupa msaada kifedha," alisema Kayombo.

Mkurugenzi huyo alisema, kodi ambazo zinalipwa zimekuwa zikitumika kutekeleza miradi ya maendeleo kama ya barabara, maji, afya, umwagiliaji na mingine.

"Mwaka wa fedha 2022/23 tunatarajia kukusanya Sh. trilioni 23.1 na tunaona lengo linaenda kutimia Juni 30, tutaweka taarifa rasmi ya ukusanyaji wetu mambo yatakuwa mazuri," alisema.

"Mfano hapa Dar es Salaam wilaya tumezipa mamlaka ya kimkoa na tumefungua ofisi zingine kama Mbezi, Shekilango, Mbagala na kwingineko, hivyo tunaenda vizuri," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema eneo lingine ambalo limetoa matokeo chanya ni matumizi ya mfumo kidijitali na kufanikiwa kupunguza gharama kwa mlipakodi kwenda ofisini kulipa kodi na kuacha biashara yake.

"Mfumo wa kidijitali umekata mzizi wa vishoka na umepunguza gharama kwa walipakodi, hivyo tunataka kuendelea kuboresha," alisema.

# TVS India yaipongeza serikali uwekezaji

**Na Halfani Chusi**

KAMPUNI ya Pikipiki za Biashara TVS, imeipongeza serikali kwa kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji akisema hatua hiyo itachangia waendelee kufurahia kufanya uwekezaji wa bidhaa hiyo nchini.

Hayo yalisemwa jana jijini Dar es Salaam na Makamu wa Rais wa TVS, Rahul Nayak, kutoka makao makuu ya pikipiki hizo nchini India alipofanya ziara ya kutembelea biashara hiyo nchini.

Katika ziara hiyo, aliwatembelea mawakala usambazaji na uuzaji wa pikipiki hizo kusikiliza shida zinazoibuliwa na wateja wake, kwaajili ya kwenda kuzifanyia maboresho.

Alisema mteja atakayenunua pikipiki zao atapata unafuu mkubwa ikiwamo, ulaji mdogo wa mafuta ikilinganishwa na pikipiki nyingine pamoja na huduma maalumu ya kifurushi cha Rider cover kwaajili ya kumsaidia dereva anapopata ajali au ulemavu wa kudumu. "Tanzania ni pazuri, ni nchi yenye amani, na mazingira mazuri kwa biashara, serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, imeweka mazingira mazuri kwa wawekezaji tofauti na kipindi cha nyuma Malamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), wamekuwa msaada mkubwa kwetu kibiashara," alisifu.

Mkuu wa Biashara TVS, Jonathan Masanja, alisema kampuni yao itaendelea kutanua wigo wa upatikanaji ya huduma hiyo kwenye mikoa mingine.

"Kaulimbiu yetu 'Mteja wangu ni mfalme' lengo letu tunataka mteja asipate shida yoyote kuanzia kwenye spea kila kitu kiwe rahisi kupatikana.

"Pia, leo tumezindua duka kubwa la spea za pikipiki Kariakoo kwa hiyo ninawaomba watu wachangamkie fursa kwa kuja kujipatia kwa bei ya jumla na rejareja," alisema.

## KABWELA — Na Fadhili Mohammed



## Wafanyabiashara kortini tuhuma kujipatia mil. 658/-

**Na Kulwa Mzee**

WAFANYABIASHARA wawili wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu kwa tuhuma za kujipatia Sh. milioni 658 kwa ulaghai na kutakatisha fedha hizo.

Washtakiwa hao, Ridhaa Shabani na Moses Nassoro, wamepandishwa kizimbani jana na kusomewa mashtaka 11 yanayowakabili mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Rhoda Ndimilanga.

Akisoma Mashtaka, Wakili wa Serikali, Eric Davies, akisaidiana na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Grace Mwanga, alidai washtakiwa walitenda makosa hayo kati ya Agosti 28 na Septemba 9, mwaka 2022 katika maeneo tofauti nchini.

Inadaiwa katika kipindi hicho washtakiwa walikula njama ya kutenda kosa la kujipatia Sh. 658,800,400 kwa njia ya udanganyifu. Imedaiwa washtakiwa walijipatia fedha hizo kutoka kwa Reymond Mavika kwa madai watawekeza katika biashara ya mazao ya kilimo.

Katika shtaka lingine washtakiwa wanadaiwa walitakatisha fedha hizo kwa kujinunulia vitu mbalimbali huku wakijua fedha hizo ni mazalia ya kosa la kujipatia fedha kwa udanganyifu.

Mshtakiwa Shabani anadaiwa alizitumia fedha hizo kwa kununua gari aina ya Toyota IST, Music System, gari aina ya Hash, seti ya luninga, jenereta, taa za disko, trekta na Sh. milioni 21.4, aliziweka katika akaunti yake ya CRDB. Mshtakiwa Nassoro, anadaiwa alizitumia kwa kununua gari aina ya Toyota Harrier, town hiace, vipuri vya gari na Sh. milioni 96 alikutwa amezihifadhi nyumbani kwake Mang'ula, Kilombelo huku akijua ni kosa.

Hata hivyo, baada ya kuwasomea mashtaka, upande wa Jamhuri ulidai upelelezi haujakamilika.

Shauri liliahirishwa hadi Juni 21, mwaka huu na washitakiwa wote walipelekwa mahabusu.



Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Manny Ramos (wapili kushoto), akisaini mkataba wa makubaliano na Mkurugenzi Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Solomon Kimilike (wa pili kulia) na Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, Wilbard Bambara (kulia), kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) kwa mwaka 2023, wilayani Ngara, mkoani Kagera jana. Kushoto ni Kiongozi wa kitengo cha Maendeleo ya Jamii Tembo Nickel, Gervas Patrick. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

# Tembo Nickel kujenga miradi ya mamilioni afya, elimu

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

KAMPUNI ya Tembo Nickel, imesaini Mkataba wa Makubaliano (MoU) na Halmashauri ya Wilaya ya Ngara, juu ya utekelezaji wa miradi ya Uwajibikaji wa Kampuni kwa Jamii (CSR) kwa mwaka 2023 wenye thamani ya Sh. milioni 257.69.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Tembo Nickel, Manny Ramos, akizungumza kabla ya utiaji saini wa mkataba huo, alisema miradi itakayotekelezwa ni ya afya na elimu.

"Jambo hili kubwa linakuja chini ya mwezi mmoja tangu Tembo Nickel ilivyokabidhi kwa mafanikio makubwa miradi ya mwaka 2022 ya CSR. Miradi hii iligharimu Sh. milioni 208.

"Tunasimama hapa leo kwa uaminifu na manufaa kwa pande zote mbili, kuchangia kwenye maendeleo ya jamii zetu, kupitia uwekezaji wa kijamii na maendeleo ya kiuchumi yenye tija, kwa mfumo wa uwajibikaji wa kampuni kwa jamii," alisema Ramos.

Alisema Tembo Nickel itachangia katika miradi 10 ambapo tisa ipo kwenye sekta ya elimu, huku mmoja ukiwa wa afya.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na ujenzi, ukamilishaji na ukarabati wa madarasa ya shule za msingi nane, ununuzi wa madawati 225 ya shule za msingi, ununuzi wa viti 80 na meza 80 za shule ya sekondari Rulenge pamoja na ujenzi wa vyoo viwili vya kisasa vya shule za msingi kila kimoja kikiwa na matundu nane huku kwenye afya ikiwa ni ujenzi wa wodi ya kisasa ya wazazi.

Kwa upande wa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Ngara, Solomoni Kimilike, alisema uibuaji wa miradi hiyo ulikuwa wa njia shirikishi kuanzia ngazi ya jamii ambapo wao ndiyo walieleza vipaumbele vyao.

"Tulianza kuibua miradi kutoka kwa ngazi ya jamii, ikapanda kwenye vijiji, kata, wataalamu wa halmashauri na pia madiwani. Vipaumbele vilikuwa ni afya na elimu kwa hiyo miradi yote hii imefikiwa kwa njia shirikishi," alisema Kimilike.

Alisema miradi hiyo itapunguza changamoto nyingi, kwasababu imegusa maeneo ambayo yalikuwa na uhitaji mkubwa hivyo wanatarajia itakamilika kwa wakati kama walivyokubaliana.

"Tunajipanga kushirikiana na wenzetu ili ifikapo Desemba miradi yote iwe imekamilika kama ilivyopangwa, tunafurahi kwasababu wawakilishi wa wananchi wapo kwa maana watendaji na wenyeviti wa vijiji nao hapa leo wamesaini hii mikataba, kwa maana hiyo wanatakiwa kushiriki kikamilifu ili miradi ikamilike kwa ubora na kwa muda uliopangwa," alisema.

Kwa upande wa Ofisa Tawala wa Wilaya ya Ngara, Vedastus Tibaijuka, aliyemuwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Matius Kahabi, kwenye shughuli hiyo, alisema ni matarajio yao kuona miradi hiyo inatekelezwa kwa uadilifu.

Mganga Mfawidhi wa Zahanati ya Mumiramira, Halima Iddi, alisema kujengwa kwa wodi ya kinamama katika zahanati hiyo iliyo kwenye Kijiji cha Mumiramira, Kata ya Bugarama, kutaokoa maisha yao.

"Tunashukuru kwa jengo la mama na mtoto, kitu Tembo Nickel walichotufanyia ni kizuri sana, tunashukuru kwa ujio wao kwenye maeneo yetu. Ukiangalia kwenye mkataba uliosainiwa leo, sisi ndio tumetengewa fedha nyingi, niwaambie tu kwamba mradi huu ni mkombozi kwa wanawake wa kijiji chetu na kata kwa ujumla," alisema.

Mkuu wa Shule ya Sekondari ya Chifu Nsolo, Kata ya Bugarama, God Salvatory, alisema anaamini tatizo la maji shuleni kwake litaisha baada ya kupata ufadhili huo wa ujenzi wa miundombinu ya kuteka maji ya mvua shuleni hapo na tangi kubwa la kuhifadhia maji.

# Shule ya Samia waomba utatuzi ukosefu vitabu

**Na Beatrice Moses,** RUFIJI

WANAFUNZI wa Sekondari ya Wasichana ya Samia Suluhu Hassan, wameomba kusaidiwa kutatua tatizo la kukosekana kwa vitabu shuleni hapo, hali inayotishia ufaulu kimasomo.

Akizungumza kwa niaba ya wanafunzi wenzake, Shymaa Ponela, alisema uhaba wa vitabu na maji yanayopatikana shuleni hapo yana chumvi ambayo hayafai kunywa wala kuoga, lakini wanalazimika kuyatumia.

Alitoa kero hiyo mbele ya watendaji kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Kamati ya Usimamizi wa miradi, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) Zanzibar, waliofanya ziara shuleni hapo.

Mkuu wa sekondari hiyo, Rose Ushaki, alisema wanafunzi wa shule hiyo ni wenye ufaulu wa juu wa alama A, mchepuo wa Sayansi na kuwa na jukumu kubwa la kuhakikisha wanaendeleza ufaulu huo.

"Ni Sekondari mpya ya bweni, tunataraji tukifungua shule Julai kutakuwa na maboresho kwa baadhi ya mambo," alisema Ushaki.

Watendaji na Kamati hiyo wametembelea Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani, ili kujionea miradi ya miundombinu iliyotekelezwa na TASAF ili kujifunza mambo kadhaa.

Mratibu kutoka Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais Zanzibar, Makame Ally Haji, alisema wanaamini sekondari hiyo itakuwa nzuri na itatoa wahitimu ambao baadhi yao watakuwa viongozi wazuri wenye kuleta maendeleo nchini.

Alisema wameona miradi miwili iliyotekelezwa na TASAF ya Soko Kuu la Utete na Mai wa madarasa manne, matundu nane ya vyoo na ujenzi wa bweni kwenye shule hiyo.

Awali, akitoa taarifa ya ujenzi wa soko Kuu la Utete Mtendaji wa Kata ya Utete, Edmund Marcell, alisema halmashauri hiyo ilipokea zaidi ya Sh. milioni 125 toka TASAF kwa ajili ya ujenzi wa soko hilo ulioanza Februari 9, mwaka jana.

"Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji kutokana na mapato yake ya ndani iliongeza Sh. milioni 46 zilizotumika kwenye hatua ya umalizaji wa soko pamoja na ujenzi wa choo," alisema.

Marcell alisema pia wananchi wa Kata ya Utete walishiriki kufanya shughuli mbalimbali wakati wa ujenzi wa soko zilizokadiriwa kuwa Sh. milioni 2.7 na kufanya jumla ya gharama za mradi kuwa zaidi ya Sh. milioni 174.

Mratibu wa TASAF wilaya hiyo ya Rufiji, Pamella Birukila alisema halmashauri hiyo imeendelea na utekelezaji wa miradi ya miundombinu inayotekelezeka katika kata ya Mgomba na Utete.

"Miradi hii imetekelezwa ikiwa ni hitaji la jamii baada ya miundombinu iliyopo kuwa imechakaa au kutokuwapo.

Sh. milioni 361 zimepokewa na Halmashauri ya Wilaya ya Rufiji zikiwa ni kwa ajili ya miradi ya miundombinu," alisema.

# Wataka sheria ndogo uchangiaji damu

**Na Mary Mosha,** MOSHI

MWAMKO mdogo wa uchangiaji damu nchini umewaibua wanafunzi wa vyuo vya elimu ya juu mkoani Kilimanjaro wakiishauri Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Wizara ya Afya, kuja na mwongozo maalum utakaozisukuma halmashauri za wilaya kutunga sheria ndogo ya kuchangia damu.

Wazo la kutaka kutungwa sheria ndogo ya kuwabana wenye sifa kuchangia damu lilitolewa jana katika Manispaa ya Moshi na wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MoCU) wakati wa kampeni ya uchangiaji wa damu.

Akieleza kuhusu umuhimu wa sheria hiyo, Honest Lyimo, mmoja wa wanafunzi hao, alisema ni lazima kuchangia damu ili kuhakikisha wenye uhitaji wanaendelea kuishi.

Alionya kuwa uchangiaji damu kufanywa kuwa hiari, ni hatari na anaona kuna haja suala hilo litazamwe vizuri kitaifa.

Esau Massawe mwanafunzi mwingine chuoni huko, alisema ili kulifanya suala la uchangiaji damu kuwa la lazima, serikali isisite kuagiza mabaraza ya madiwani katika kila halmashauri nchini, kutunga sheria hiyo ili kuongeza mwitikio wa watu kujitokeza kuchangia damu.

Kwa mujibu wa Mpango wa Taifa wa Damu Salama (NBTS), sifa za mtu anayeweza kuchangia damu ni yeyote asiye na maradhi kama vile kisukari, shinikizo la damu, kifafa, ugonjwa wa ngozi na asiwe mjamzito au anayenyonyesha.

Mpango huo pia unaweka masharti ya asiwe na mwenendo unaoweza kuhatarisha kupata maradhi yanayoambukizwa kwa njia ya damu (kufanya ngono zisizo salama, kutumia dawa za kulevya, ulevi wa kupindukia), awe na umri kati ya miaka 18 hadi 65, uzito wa kilogramu 50 au zaidi na asiwe katika tiba yoyote.

Ofisa Uhamasishaji wa Benki ya Damu Salama Kanda ya Kaskazini, Feisal Abubakar, akizungumzia kampeni hiyo, alisema ili kukabiliana na upungufu wa damu salama katika vituo mbalimbali vya kutolea huduma za afya, Kituo cha Ukusanyaji Damu Salama Moshi kimelenga kukusanya chupa za damu 875 kwa siku 14 ili kukabiliana na upungufu wa damu uliopo.

"Tumeanzisha kampeni ya siku 14 kuanzia Juni Mosi hadi 14 mwaka huu na tumelenga kila siku angalau tukusanye chupa 60 za damu ili tutakapofika Juni 14, ambayo ni siku ya uchangiaji damu duniani, tuwe tumekusanya chupa za damu 875.

Kanzidata ya kituo hicho inaonyesha kuwa kuanzia mwezi Julai mwaka jana hadi Mei 31 mwaka huu, wamekusanya chupa za damu 8,098 kati ya 12,504 walizokuwa wamepanga kukusanya kwa mwaka mzima, sawa na asilimia 64.7.

# Kesi kupinga tangazo la waziri yawekewa mkakati

**Na Tumaini Mafie,** ARUSHA

KESI ya kupinga tangazo la Waziri wa Maliasili la kuitwaa ardhi ya wanavijiji wa Loliondo mkoani Arudha kuwa eneo la Pori Tengefu la Pololeti, imepangwa kusikilizwa kwa njia ya maandishi na Mahakama Kuu Kanda ya Arusha Julai 31 mwaka huu.

Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Joachim Tiganga ambaye anasikiliza kesi hiyo, ameridhia shauri hilo kuanza kusikilizwa kwa njia ya maandishi ili kukabiliana na tatizo la muda.

Kutokana na hoja hiyo iliyowasilishwa na upande wa waleta maombi, Jaji Tiganga alisema waleta maombi wanapaswa kuwasilisha hoja zao Juni 18 mwaka huu, na hoja za nyongeza zinapaswa ziwasilishwe Julai 23 mwaka huu.

Kesi hiyo namba 21 ya mwaka 2022, ilifunguliwa mahakamani humo kama maombi ya mapitio ya sheria (Judicial Review Application) dhidi ya tangazo la Waziri wa Maliasili na Utalii kupitia (GN No 421 ya Juni 17).

Katika shauri hilo, waleta maombi watano kutoka vijiji vilivyoathirika, wanaiomba mahakama iagize serikali kuondoa zuio dhidi ya wananchi kuingia katika eneo la Km zaq mrada 21,502, ambalo wamekuwa wakitumia kwa ajii ya malisho ya mifugo yao na kufanyia shughuli za imani yao.

Pili, wanaiomba mahakama itengue tangazo la serikali (GN 421) la Juni 17, 2022, kwamba ni batili na lilitangazwa kinyume cha sheria na halikuwashirikisha wananchi kama sheria inavyotaka.

Tatu, wananchi hao wanaiomba mahakama hiyo itamke kuzuia serikali na mawakala wake wasifanye oparesheni zote katika eneo hilo.

Jopo la Mawakili linalowawakilisha waleta maombi katika kesi hiyo, linaongozwa na Mpale Mpoki, Jeremiah Mtobesya, Dennis Mosses na Yonas Masiaya, huku upande wa Jamhuri ukiongozwa na Wakili Peter Mseti anayesaidiwa na Jackline Kinyasi.

Kabla ya Jaji Tiganga kuridhia hoja hiyo ya kisheria, Wakili Mpoki alidai kuwa kutokana na hoja ya muda, wanaomba shauri hilo lisikilizwe kwa njia ya maandishi kwa muda wa wiki tatu.



Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Sokoni, Kata ya Majengo, Manispaa ya Moshi, Daima Kapongo (kushoto), akipanda mti pamoja na Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la Mongola Environment and Conservation Group (MECG) katika kata hiyo ikiwa ni sehemu ya shughuli za shirika hilo kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani mapema wiki hii. **PICHA: JAMES LANKA.**

# Beng'i ajivunia mradi wa Rais Samia usawa kiuchumi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC), Beng'i Issa, amesema Rais Samia Suluhu Hassan ameanzisha mpango maalum unaoitwa Generation Quality Forum, ukilenga kuleta usawa wa kiuchumi kwa wanaume na wanawake.

Beng'i alikuwa akizungumza jana katika Manispaa ya Moshi wakati wa mafunzo ya urasimishaji na uendelezaji wa biashara kwa wanawake na vijana Mkoa wa Kilimanjaro yaliyotolewa chini ya Shirika la KWIECO.

Mradi wa Mwanamke Imara unatekelezwa na Chama cha Wanasheria Wanawake Tanzania (TAWLA), Mtandao wa Mashirika Yanayotoa Huduma ya Msaada wa Kisheria Tanzania (TANLAP), Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Barani Afrika (WiLDAF) na Shirika la Kilimanjaro Women Information Exchange & Community Organization (KWIECO).

"Nia yake (Rais Samia), ni kuleta usawa wa kiuchumi kwa wanaume na wanawake; kwa sababu wanawake tumeachwa nyuma kiuchumi kwa muda mrefu, mambo mengi sasa kupitia jukwaa hilo yatawasaidia kuongeza thamani ya uchumi wenu na maisha yenu," alisema.

Katibu Mtendaji huyo wa NEEC alisema ili mtu yeyote athaminike katika jamii na hata familia yake, ni lazima uchumi wake ukae vizuri.

"...Ili upate thawabu kwa Mungu, ni lazima uchumi wako ukae vizuri ili usifanye dhambi ndogo ndogo. Lakini ukiwa umekaa vizuri kiuchumi, utapunguza hata kutenda dhambi. Ni rahisi sana wanawake ambao hawako vizuri kiuchumi kuonewa na ni rahisi sana kukosa kujiamini," alisema Beng'i.

Kuhusu ongezeko la kasi la uanzishwaji wa taasisi za mikopo mitaani, maarufu kausha damu, Beng'i alisema:

"Kuna hizi taasisi ambazo zimeanzishwa sasa hivi zinaitwa kausha damu, si mnazijua? Ni taasisi za kuangalia sana, kwa sababu riba yake ni kubwa ambayo wanatutoza. Wewe kwa sababu hujui, ndio maana wanakuambia mkopo wako, ukiomba leo utapata kesho. Na kweli unapata lakini utakuja kulipa asilimia 100."

Awali, Mratibu wa Mradi wa Mwanamke Imara, Stuart Nathaniel, alisema unatekelezwa katika wilaya sita na halmashauri saba.

"Katika Mkoa wa Mbeya, tupo Wilaya za Rungwe, Mbarali, Rungwe na Mkoa wa Njombe tupo Ludewa na Makate. Wakati Kilimanjaro tupo Wilaya za Rombo na Moshi," alisema Stuart.



# Wakulima walia na kushuka bei pamba

**Na Daniel Limbe,** CHATO

BAADHI ya wakulima wa pamba wilayani Chato mkoani Geita wamelalamikia kushuka kwa bei ya zao hilo, wakidai imeshuka kwa zaidi ya Sh. 700 kwa kilo kulinganisha na bei ya msimu uliopita.

Wamesema bei ya pamba imeshuka kutoka Sh. 1,800 kwa kilo moja msimu wa mwaka 2022/23 hadi kufikia Sh. 1,060 msimu huu.

Wameitaja ni hali inayowakatisha tamaa baadhi yao kulima zao hilo kutokana na hasara wanayotarajia kuipata kutokana na gharama kubwa walizotumia katika uzalishaji, huku baadhi yao wakiomba serikali kuzishinikiza kampuni za ununuzi wa zao hilo kuongeza bei itakayomnufaisha mkulima.

Wakizungumza na Nipashe jana, wakulima hao akiwamo Nelson Mayeka, walisema bei ya 1,060 iliyopo katika vituo vya kununulia pamba wilayani Chato inakatisha tamaa ya kuendelea na kilimo hicho.

Walisema wakulima wengi walihamasika kulima zao hilo baada ya msimu wa mwaka 2022/23 pamba yao kununuliwa kati ya Sh. 1,600 na 2,000 kulinganisha na msimu huu.

Onesmo Hoja, mkulima wa pamba, alisema katika kuhakikisha wanavuna pamba bora, wanaingia gharama kubwa tofauti na bei walizopangiwa, hali inayotarajiwa kuwasababishia hasara katika kilimo hicho.

Ofisa Ushirika Wilaya ya Chato, Deograthias Bundala, aliwataka wakulima kuzingatia usafi wa pamba kuanzia mashambani hadi vituo vya kuuzia pamba na kuacha kutumia vifungashio vya mifuko ya sandarusi, kuweka mchanga, mafuta ya kenge na mawe na maji.

Alisema tabia hizo zinahatarisha ubora wa zao hilo. Wakiacha tabia hizo, kutasaidia kupatikana bei nzuri katika soko.

Ofisa Kilimo Kata ya Chato, Evelline Kamzola,alizihakikishia kampuni zote zitakazonunua pamba wilayani hapa kuwa zitapata pamba yenye ubora kutokana na usimamizi na maelekezo mazuri waliyopata wakulima tangu kuandaa mashamba, kulima, kuchambua hadi kuuza zao hilo, huku akiwaonya baadhi ya wakulima wenye lengo la kuchafua pamba ili kujiongezea uzito kinyume cha sheria.

# Fimbo ya kichwani iliyoua ilivyompeleka jela miaka 8

**Na Halima Ikunji,** TABORA

ADELA Haruna (40), mkazi wa Mtaa wa Nyerere, Manispaa ya Tabora, amekuhumiwa kwenda jela kutumikia kifungo cha miaka minane kwa kosa la kumuua Sadiki Tito bila kukusudia kwa kumpiga na fimbo kichwani na kumsababishia kifo.

Kitendo hicho ni kinyume cha kifungu namba 195 na 198 Sura ya 16 ya Sheria ya Kanuni za Adhabu iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2019.

Hukumu hiyo ilitolewa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama Kuu Kanda ya Tabora, Athumani Matuma, aliyeeleza kuwa mshtakiwa huyo alikutwa na hatia kwa kufanya mauaji hayo.

Alisema kuwa ugomvi ulikuwa sio wa kwakem bali wa marehemu na mtoto wake, Haruna Matias katika tukio lililotokea Machi 22 mwaka huu.

Jaji Athumani alisema mshtakiwa aliamua kuingilia ugomvi kwa kuwaadhibu wagombanao wote wawili ambao ni marehemu na mtoto wake kwa kumtandika marehemu fimbo za kichwani, hivyo kumsabashia kifo. Alieleza kuwa taarifa za awali kutoka kwa daktari zilionyesha marehemu alipata majeraha mbalimbali kichwani na mkono wa kushoto.

Wakili wa Utetezi, Flavia Francis, aliiomba mahakama impunguzie adhabu kutokana na kukiri kosa lake na kutokuichelewesha mahakama na kuwa kosa lake ni la kwanza. Mahakama hiyo ilizingatia ombi hilo na kumpatia adhabu ya kifungo cha miaka minane.

Kabla ya hukumu hiyo kutolewa, Upande wa Jamhuri ulikuwa na Mawakili Robert Kumwembe, Ida Rukangira, Oresta Kemilembe, Aziza Mfinanga, uliiombia mahakama hiyo itoe adhabu kali dhidi ya mshtakiwa ili iwe fundisho kwa watu wengine.




Wajumbe wa Kamati ya Siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Shinyanga Vijijini, wakitembelea kuangalia utekelezaji wa miradi ya maji inayotekelezwa na Mamlaka ya Maji Shinyanga (SHUWASA), katika kijiji cha Didia wilayani humo juzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Mgodi wajitosa kusaidia vifaa huduma za uzazi vituo vya afya

**Na Mwandishi Wetu,** GEITA

KAMPUNI ya Geita Gold Mining Limited (GGML) imetoa msaada wa vitanda vinne kwa ajili ya kujifungulia katika Vituo vya Afya Nyankumbu na Kasamwa, Halmashauri ya Mji wa Geita mkoani Geita.

Msaada huo ulikabidhiwa wiki iliyopita na Meneja Mwandamizi Uhusiano wa GGML, Gilbert Mworia kwa niaba ya wafanyakazi wanawake wa kampuni hiyo baada ya kupokea ombi la vituo hivyo vya afya kuhusu upungufu wa vitanda hivyo.

Alisema katika maadhimisho ya Siku ya Wanawake iliyofanyika Machi mwaka huu, kampuni hiyo ilipokea ombi kuhusu uhaba wa vitanda vya kujifungulia kutoka kwa wanawake wa eneo hilo.

Mworia aliongeza kuwa suala la afya na ustawi wa jamii ni muhimu katika kila hatua ya maisha ya mtu yeyote anayekua na ndiyo maana GGML imeendelea kuboresha huduma za afya katika jamii inayozunguka mgodi huo na Tanzania kwa ujumla.

"Leo tunakabidhi rasmi vitanda hivi ambavyo wazo lake lilitokana na adha wanazopata kinamama wakati wa kujifungua. Waliwasilisha hili kwa menejimenti na sasa tumechukua hatua ipasavyo kwa kusikia kilio chao," alisema.

Aikizungumza katika hafla ya makabidhiano ya vitandani hivyo, Mkuu wa Wilaya ya Geita, Kanali Boniphace Maghembe, aliagiza timu ya madaktari wa Vituo vya Afya Kasamwa na Nyankumbu kutunza vitanda hivyo vya kujifungulia vilivyotolewa.

"Hatupati msaada wa aina hii mara kwa mara, hivyo ninawahimiza kila mmoja wenu hapa kuhakikisha anatoa kipaumbele katika utunzaji mzuri wa vitanda hivi vilivyotolewa na GGML," aliagiza.

Mganga Mfawidhi wa Kituo cha Afya cha Nyankumbu, Irene Temba, alipongeza GGML kwa msaada huo na kubainisha kuwa kituo hicho kimekuwa kikikabiliwa na changamoto nyingi hususani katika upande wa huduma ya kujifungua.

"Tunarekodi watoto wasiopungua 300 kila mwezi, jambo ambalo huwalazimu baadhi ya mama zetu kutumia vitanda vya kawaida wakati wa kujifungua.

"Tungependa katika siku za usoni, GGML ifikirie pia kutusaidia na vitanda vya kufanyia uchunguzi, samani na vifaa vingine kwa sababu kila mwezi hapa tunapokea zaidi ya kesi 1,000 za huduma ya afya ya uzazi na ujauzito.

Pia tunatoa huduma kwa watu 1,000 kila mwezi katika Kituo cha Matunzo na Tiba," alisema.

Mmoja wa wanufaika wa awamu ya pili ya vitanda vya kujifungulia katika Kituo cha Afya Kasamwa, Mganga Mfawidhi Thomas Mafuru, pia alipongeza GGML kwa kuisaidia Kasamwa.

"GGML ni rafiki mkubwa wa Kituo cha Afya Kasamwa. Tangu kituo kilipoanzishwa mwaka 2007, GGML imetoa msaada wenye thamani kubwa ikiwa ni pamoja na usambazaji wa vifaa vya afya na hata ujenzi wa uzio kuzunguka kituo chetu," alisema.

GGML imekuwa kinara wa uwekezaji katika jamii tangu ilipoanzishwa mwaka 2000, huku vipaumbele vikubwa vya kampuni hiyo vikiwa ni afya, elimu, maji, barabara na miradi ya maendeleo na miradi mingine ya kijamii inayolenga kuboresha ustawi wa jamii inayozunguka mgodi.



Ukurasa 12

SACP Mutafungwa katua Mwanza akipasafisha wahalifu hadi barabarani, mauzo yaneemeke




Ukurasa 13

Watanzania tunaacha mbachao tu, kwa msala upitao!

BUFE
IJUMAA JUNI 9, 2023
Nipashe



Ukurasa 14

**MARSHALL MBISE**
**Mama mwenye ulemavu miaka 23 katika mapambano magumu kujikimu**

# Mshika usukani wa awamu ya sita anavyovaa viatu uchumi vya JPM

**Na Halfani Chusi**

ULIPOTOKEA msiba wa nchi kupoteza Rais Dk. John Pombe Magufui miaka miwili na robo iliyopita, hofu na majonzi yalitanda nchi nzima.

Ni usiku huohuo, umma ukapewa mrejesho wa kwamba watulie, sauti kutoka kwake Makamu wa Rais, Dk Samia Suluhu Hassan, kwamba nchi iko salama na anabeba jukumu la malezi.

Kimsingi, kupata kwake nafasi uongozi ngazi ya juu kitaifa, kuliambatana na majonzi ghafla, ikiwa tofauti na watangulizi wote kwenye nafasi hiyo waliopokea kwa furaha katika awamu nyingine tano nchini.

Kadri siku zilivyosonga, Watanzania wakashuhudia mambo kadhaa yaliyowainua kiimani, kama alivyoahidi katika hotuba yake Rais Dk Samia.



Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.



Mkuu wa nchi wa awamu ya tano, marehemu Dk. John Magufuli. **PICHA ZOTE: MAKTABA.**

Kama ambavyo ingemkuta yeyote anayepokea madaraka hayo chini ya kofia ileile alikotokea kuwa msaidizi wa mkuu wa nchi kiserikali na mnyororo uleule wa chama tawala - CCM ‘wakijenga nyumba’ ileile, Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akaahidi kuendeleza waliyoyaanzisha.

Ni baada ya muda mfupi kukaoneka ‘matofali’ na ‘lipu’ zikiboreshwa kuendeleza miradi mikubwa iliyoanzishwa, ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa ambao wiki hii imepokea mabehewa mapya ya kisasa, hali kadhalika mradi mkubwa wa umeme wa Mwalimu Nyerere, unaoendelea kufanyiwa kazi, sasa ukiwa hatua za mwisho.

Ni dhana pana inayoangukia nadharia ya uchumi wa maendeleo, unaonena tafsiri pana ya kujenga miundombinu ya mabadiliko ya tija kwenye ubora na wingi wa miundombinu inayounda hatua za kuendelea, katika sekta tofauti.

Ndani ya miaka miwili ya utendaji wa Rais Dk. Samia, sura ya mavuno inashuhudiwa kwa wawekezaji na wengine wapya wakija kwa kasi, kufunguliwa kampuni zilizofungwa, pamoja na miongozo bora na rafiki kwa wawekezaji nchini.

Eneo mojawapo la mfano ni kwenye suala la umeme vijijini, mradi ulioanza awamu nyinginezo na bado unaendelezwa kwa ufanisi kufikisha nishati hiyo umma uliko, ndani ya awamu sita za uongozi wa nchi, asilimia kubwa ya vijiji utawala wake umefikiwa na huduma hiyo, mipango mingine mingi ikiwa jikoni.

Simulizi nyingine inaangukia katika sekta kilimo na miundombinu yake, ikiwamo mipango ya umwagiliaji, sambamba na kurahisishwa upatikanaji mikopo kwa wakulima kwa riba nafuu.

Kwa sasa ndio sura ya awamu iliyoko kiserikali chini ya Rais Dk. Samia, wakulima wananufaika sasa kuhudumia maeneo makubwa, huku kukifunguliwa mianya ya kuuza mazao katika masoko ya kigeni, ambayo tafsiri yake pana ni kusaidia kuongeza soko na upatikanaji ajira kwa wakulima.

**MIPANGO HADI VITENDO**

Dhamira mojawapo katika matendo inajitokeza Rais Dk. Samia, akiwa ziarani mkoani Kagera, anapowataka viongozi wa mkoa kutenga maeneo makubwa ya kilimo hekta 70 kwa ajili ya kuzalisha alizeti, ili kuwezesha upatikanaji mafuta ya kula nchini na kuondoa utegemezi nje ya nchi.

“Tanzania tumekuwa tukitegemea mafuta ya kula kutoka nje, lakini kutokana na janga la Uviko-19, tumepata tatizo la kukosa mafuta baada ya kufungwa mipaka, hivyo hatuna budi kufanya uzalishaji wa ndani na ili tujitosheleze lazima tuwe na mashamba makubwa ya alizeti pamoja na michikichi,” akatamka rais.

Hadi sasa kuna hatua inashuhudiwa kupigwa katika eneo hilo tangu wito wa kiserikali uanze kutolewa, kukijengwa viwanda vya kati binafsi vya kuzalisha mafuta ya kupikia, zaidi zikitumia malighafi alizeti ya nchini, hasa katika mikoa ya Singida, Mwanza na Dar es Salaam.

Katika kile kinachoonekana kuboresha mipango ya maendeleo kitaifa, hivi karibuni kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wafanyakazi kitaifa, akatamka kuwaongezea mishahara wafanyakazi, jambo ambalo wengi wamelisubiri kwa shauku, huku Rais Dk Samia akifafanua sasa itafanyika katika namna endelevu, kama ilivyowahi kuwapo zamani.

Ni hatua inayotajwa kuendana na ongezeko la bajeti ya fedha ya mkopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, kuwanusuru baadhi waliokosa mikopo awali, sasa neema na fursa hiyo, hatua yake ikipigwa zaidi hadi kwa wanaosoma ngazi ya diploma, ambayo haikuwapo awali.

Katika lugha nafuu, ni kwamba eneo la nguvu kazi ya Kitanzania inazidi kuboreka kwa kuelimika na inapata ufanisi maradufu.

Pia, kuna eneo la kudumisha uhusiano baina ya Tanzania na nchi jirani, kitendo kilicholeta matokeo chanya hata mtaani kwa kiasi kikubwa, vijana wengi wameanza kupata ajira kwenye taasisi mbalimbali, ikiwamo viwandani na kwenye kampuni binafsi.

Ndani ya tafsiri hiyo ya ajira, ni wiki hii kukitangazwa bungeni, serikali inaajiri watumishi wastani wa 13,000 katika kada za elimu afya na walipa kodi nao wakiondolewa kwenye ulingo wa mgogoro na wakusanya kodi, Mamlamka ya Mapato Tanzania (TRA), ukianazishwa Ofisi ta Usuluhishi wa Kodi, chini ya Wizara ya Fedha.

Vilevile, sura tofauti ya mipango maendeleo kwa wanafunzi, hatua ya kuwatetea walioshindwa ku-

INAENDELEA UK.12

BIASHARA

# SACP Mutafungwa katua Mwanza akipasafisha wahalifu hadi barabarani, mauzo yaneemeke

- Ateta na mamia wafanyabiashara, waganga jadi na sungusungu
- Kashitukia walinzi binafsi 'vimeo', wanapora vituo vya mafuta
- Upekuzi mzito kwenye vyuo vya udereva na kampuni za ulinzi

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

AMETIMIZA miezi kadhaa sasa, Kamanda wa polisi Mkoa wa Mwanza,SACP Wilbrod Mutafungwa, tangu ahamie mwishoni mwa Novemba mwaka jana.

Anakitaja kipindi hicho kilikuwa cha hekaheka kuelekea Sikukuu za krismasi na mwaka mpya, ni historia yake fupi aliyoitoa katika mazungumzo maalum na Nipashe, kuhusu utekelezaji wa majukumu yake ya kila siku.

Kamanda SACP Mutafungwa, anaeleza namna anavyotumia ofisi yake kujipanga awezeshe ustawi wa shughuli za kiuchumi na biashara mkoani Mwanza.

Afande Mutafungwa, ambaye si mgeni na cheo cha 'RPC' na awali alikuwa Kamanda wa Polisi wa Usalama Barabarani, anataja jambo aliloanza kulitekeleza mkoani Mwanza, ni kuhakikisha usalama wa watu na mali zao, kuwezesha shughuli zao zinabaki katika usalama amani na utulivu mkubwa.

Anasema akaanza kwa kukutana na makundi mbalimbali ya wananchi, kwa ajili ya kufanya uwezeshaji mkubwa kuwashawishi, kuwajengea uwezo ili waweze kushirikiana na jeshi la polisi kuwapatia taarifa za kihalifu na wahalifu.

Katika kulitekeleza, akashirikisha kwa karibu madawati ya uelimishaji ndani ya jeshi hilo, katika ngazi za wilaya na mkoa, akizunguka maeneo yote na makundi mbalimbali.

"Makundi niliyokutana nayo ni wafanyabiashara wa



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbrod Mutafungwa. **PICHA ZOTE: ANTHONY GERVAS.**

jiji la Mwanza,wapatao 400, wenye maduka makubwa ya biashara mbalimbali,ambao walinipa changamoto zinazowakabili kutokana na matukio ya kihalifu," anasema Mutafungwa.

Vilevile, anataja makundi ya viongozi ulinzi wa jadi Sungusungu, katika wilaya za Kwimba, Misungwi na Magu, ambao wapo kwa ajili ya kutatua migogoro ya kudhibiti mauaji yatokanayo na imani za kishirikina, ikiwamo migogano ya mipaka ya ardhi.

Anataja kundi jingine la wanaofanya biashara za uganga wa jadi wakiwapo 380 mkoani humo kikao kilichofanyika jijini Mwanza, akisema dawati la uelimishaji kupitia kitengo cha upelelezi, anataja ndicho kinahusika mkoani Mwanza, ili kiendelee kubaki salama.

Pia, anasema amewaagiza wakuu wa polisi wilaya zote nao waendeleze anavyofanya yeye, akisisitiza suala la ushirikishwaji jamii na kuweka mpango mahususi kuhusu kutanzua changamoto mbalimbali za uhalifu, ni muhimu kwao.

Kamanda Mutafungwa anasema, mkakati huo umemsaidia kupata undani wa changamoto katika jiografia ya mkoa wa Mwanza, hata akapata namna ya Polisi kuzama kwa kina kuzitanzua, ikishirikiana na wananchi.

Anasema hadi sasa, ameweza kufungua fursa nyingi kwa wananchi kutoa taarifa na matukio ya kihalifu ambazo sasa wanazichakata na kisha kuanza kufanya misako ya kuwatia nguvuni wahusika popote walipo.

Kamanda anasema, ni msako unaoongozwa na taarifa za wananchi, zenye mahitaji na hali halisi katika maeneo yao, badala ya kutumia nguvu, raslimali nyingi kutafuta wahalifu wakati wa doria.

Hapo anatoa mrejesho kwamba, imesaidia kukabiliana na matukio mengi mkoani humo, alipowasili Mwanza akakuta tukio la kuuawa mtu mwenye ulemavu wa ngozi wilayani Kwimba, amekatwa mkono wa kulia kutimiza imani za kishirikina.

Kamanda analieleza ni tukio hilo lililoshangaza kwa sababu watu watano waliokuwa wamehusika katika tuhuma za mauaji hayo, wakiamini ni njia ya kutajirika, wahusika wakatiwa mbaroni na polisi, kwa kushirikiana na wananchi watoa taarifa za siri.

Anasimulia kwamba ni imani ya kupata utajiri kupitia viungo vya albino, kwenye shughuli za madini, pia kilimo kingetoa mazao mengi, analolirejea likamsikitisha hata anafika hatua akajipanga kuhakikisha anakomesha matukio ya aina hiyo.

"Hivi sasa hakuna mhalifu anayetamba katika mkoa wa Mwanza, wala kunyanyua mabega kiasi cha kuwanyima raha au amani watu. Mwanza ni kubwa hata katika takwimu za Sensa ya Watu na Makazi 2021, ina zaidi ya watu milioni 3.6," anatamka SACP Mutafungwa.

Mwanza kunatajwa ni mkoa wenye watu wageni na wenyeji, wanaofanya shughuli za kiuchumi na kibiashara, huku SACP Mutafungwa akisema, polisi imeimarisha jukumu la doria kupitia magari yao, huku jamii ikiwasaidia juhudi hizo waliko kuhakikisha wanaendelea kuwa salama.

**WALINZI MAJAMBAZI**

Anataja hatua zingine walizochukua, ni kutathmini kampuni binafsi za ulinzi, akidai baadhi ya walinzi wamekuwa wakijihusisha na matukio ya kihalifu, wanatumia silaha walizopewa lindoni wanaenda nazo kwenye vituo vya mafuta na kuwapora fedha wenzao, kisha wanakimbia.

Mutafungwa anasema, walinzi wengi walibainiwa wameajiriwa bila kuwa na kumbukumbu za kutosha ulinzi wao, hivyo aliweka Dawati la Uhakiki kupitia Idara ya Upelelezi Polisi, wakahakikiwa walinzi kwenye kampuni binafsi za ulinzi, kuhusu uhalali wao.

Anasema, kwa sasa walinzi wote wameshahakikiwa kama wamepitia mafunzo ya mgambo, ili kuepuka 'makajanja' hatua za uhakiki zikishirikisha Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ili kufahamu uraia wa kila mlinzi mkoani.



Mitaa ya kibiashara jijini Mwanza.

Anasema zaidi ya kampuni 200 za ulinzi zimehakikiwa, huku jeshi la polisi likishiriki kupitia kitengo cha Dawati la Uhakiki wa Matukio ya Kihalifu.

**AJALI ZA BARABARANI.**

Kamanda Mutafungwa anasema, polisi mkoani hapa inaendelea kufuatilia na kuvikagua ama vyuo au shule za udereva, kupitia kitengo cha Usalama Barabarani, kuhusu usimamizi na namna ya leseni inavyotolewa.

Anataja lengo la ukaguzi huo ni kufahamu kiwango chao cha kutimiza vigezo na masharti ya kuwafundisha madereva hao.

Kwa mujibu wa Kamanda Mutafungwa, serikali inataka kutoa leseni kwa 'madereva bora' na sio 'bora dereva' kuepuka ajali zisizokuwa za lazima kwa wananchi. Hivyo, anasema wako chonjo kuhakikisha wanatokomeza ajali mkoani Mwanza.

"Kupitia kitengo cha Usalama Barabarani, tulivifungia vyuo 12 vya udereva katika mkoa wa Mwanza, baada ya ukaguzi huo vilivyokuwa vikiendesha mafunzo pasipo sifa, ili kudhibiti madereva wasiokuwa na sifa kuendesha magari na vyombo vingine vya moto," anasema SACP Mutafungwa.

Anaorodhesha sababu kuu za ajali barabarani zinachangiwa na rushwa, mwendokasi, ulevi wa pombe, uchovu wa dereva na ubovu wa miundombinu barabarani.

Mengine anayataja kuwa ni, ubovu wa magari, dereva kukosa umahiri barabarani, simu za mkononi na hali ya hewa.

Ili kuyakabili Mutafungwa anasema polisi imejipanga kuhakikisha inadhibiti ajali nyingi zinazotokana na madereva kutozingatia kanuni, sheria usalama barabarani na makosa ya kibinadamu, anayoyataja yanabeba asilimia kubwa ya chanzo cha ajali barabarani.

Anasema wamekuwa wakifanya kazi ya kutoa elimu kwa watoto wa shule, waendesha bodaboda, bajaji na makundi mengine yanayotumia huduma za barabara, wasimamie kanuni, sheria na taratibu kupitia elimu hiyo.

Tahadhari yake ni kwa wasioheshimu na kutii sheria bila ya shuruti, ikiwamo kutotii alama za barabarani hawawezi kuachwa nje ya hatua za kisheria.

Kamanda Mutafungwa ananyoosha kidole mahsusi kwa madereva wanaovunja sheria na hasa kwenye bodaboda wasiovaa kofia ngumu, pia wanaopita kwenye taa nyekundu bila ya kusimama, ikiwa taa zimezuia kupita, akinena Polisi Mwanza, inaendelea na oparesheni endelevu ya kuwakamata wanapovunja sheria hizo.

Anasema kundi la walioelimishwa mara nyingi zaidi kuhusu vitendo vya uvunjaji wa sheria, ni waendesha 'bodaboda', lakini wamekuwa wakaidi, hata wanasababisha ajali nyingi barabarani.

Hitimisho lake ni kwa askari wa usalama barabarani, kufanya kazi ya kusimamia sheria kwa uadilifu, vilevile kuepuka rushwa, huku doria zikiimarishwa katika barabara zote kuu zinazotoka Mwanza kwenda nje ya mkoa kama vile Musoma,Geita na Shinyanga.

# MSHIKA USUKANI WA AWAMU YA SITA ANAVYOVAA VIATU UCHUMI VYA JPM

**INATOKA UK.11**

maliza elimu shuleni kwa sababu mbalimbali, zikiwamo mimba, ada, maradhi sasa wanahakikishiwa kupata elimu kwenye shule mbalimbali.

Ni hali iliyowaibua wataalamu na wadau mbalimbali wa elimu wakisifu jitihada hizo, wakidai ni hatua nzuri itawawezesha watoto wa kike kutimiza ndoto zao na hata kuibua tabasamu kwa waliokwama njiani kielimu.

Simulizi kama hiyo, inaangukia pale mtu alipojitolea kuwa mtu wa kwanza kuchanjwa chanjo ya Uviko - 19, kwa lengo la kuwaaminisha watanzania chanjo hizo, hazina madhara kiafya na akafanya yote ili kutuokoa dhidi ya janga ambalo lilitikisa dunia.

Kwenye eneo hilo, akasimama kuwa mlezi, akijitokeza kuwa wa kwanza kuchanja katika tafsiri iko salama kwa matumizi ya umma, kwa kuhofu kudhurika.

**UCHUMI, SIASA, UTAWALA**

Nadharia nyingine katika matendo ya Dk. Samia ni pale anaoanisha siasa na utawala bora, kuwa nyenzo muhimu katika kuhuisha maendeleo ya uchumi kitaifa.

Ni hapo Rais Dk.Samia katika uamuzi, anakumbuka kwa kutoa maagizo ya haja ya polisi kuzingatia haki za mahabusu na watuhumiwa wengine, akisistiza kwamba bado ni binadamu.

Hapo akatamka: "Kama upelelezi ni mgumu kukamilika, ni heri mtu aachiwe akaendelee kufurahia uhuru wake mtaani.

Anaendelea: "Mwanadamu ni mwanadamu, naomba mkae na wadau wengine muangalie sheria ya kumuweka mtu mahabusu, kwenye nchi nyingine za wenzetu mtu hakamatwi mpaka upelelezi uwe umekamilika!

"Na akikamatwa, anakaa mahabusu wiki anapelekwa mahakamni anahukumiwa mambo mengine yanaendelea, huwezi kukuta serikali inabeba mzigo wa kulea mahabusu maelfu kwa maelfu. Naomba mliangalie hilo ili tuweze kutoa huduma njema na zinazofaa kwa watu wetu."

Ni tamko lililoendana na kufutwa zuio la vyama vya siasa kufanya mikutano ya hadhara, akilitaka Jeshi la Polisi kuwalinda na kusimamia mikutano yao, jambo lililomfanya azoe sifa ndani na nje ya nchi.

"Serikali tunawajibu wa kulinda mikutano ya vyama vya upinzani... mnatupa taarifa, vyombo vinatoa ruhusa wajibu wetu kama serikali nikuwalinda mfanye mikutano salama, muondoke salama wajibu wa vyama vya siasa ni kufuata sheria inavyoelekeza" anatamka Rais Dk. Samia.

Pia, anafunga upande wa pili wenye ustawi mkubwa katika maendeleo ya uchumi kitaifa, akihimiza kufanyika kwa siasa za kistaarabu na anakemea matusi kwenye majukwaa, akiwataka wanasiasa watumie nafasi hiyo kuikosoa serikali na kuinyoosha mahali kwenye upungufu, vyote katika sura pana vina ishara bora katika maendeleo uchumi, ikiwamo kukaribisha uwekezaji.

Leo hii hili limewafanya Watanzania kumpa jina 'Mama wa Makavu Live' wakiwa na maana ya mtu anayesema ukweli papo hapo bila kuficha na inapobidi anatenda na hata 'kutumbua' inapobidi.

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Watanzania tunaacha mbachao tu, kwa msala upitao!



**NA JOSEPH KULANGWA**
**+255 713 410008**
**(kulangwasos@gmail.com)**

HIVI karibuni nilipata heshima ya kushiriki Kongamano la Sera na Mitaala ya Elimu lililofanyika Dodoma kwa mafanikio makubwa, chini ya Waziri wa Elimu, Sayansi naTeknolojia, Profesa Adolf Mkenda.

Ni kongamano lililoshirikisha watu wa kada mbalimbali wakiwamo wahadhiri, wakufunzi, wanazuoni, wanafunzi wa elimu ya juu na ya chini, pia wananchi wa kawaida.

Kulikuwa na maprofesa na madaktari, vilevile raia wa kigeni ambao nao walishiriki kikamilifu kwenye kongamano lililokuwa na nia ya kukusanya maoni na mapendekezo.

Maoni na mapendekezo hayo ni ya kutaka kuona namna ya kuboresha sera na mitaala ya elimu nchini, ili kuendana na hali halisi, pia kuwezesha wahitimu kuchangia kikamilifu kulingana na elimu waliyopokea.

Pia, lengo ni kuona jinsi wahitimu hao wanavyoweza kutumia elimu yao kujiajiri, badala ya kusubiri kupewa ajira serikalini au katika sekta binafsi na kuondokana na dhana kuwa kusoma ni kupata ajira.

Kubwa likiwa ni kuachana na nadharia na kujiingiza zaidi katika elimu kwa vitendo, ambao elimu ya amali inatiliwa mkazo, kwani inawapa vijana stadi za maisha zaidi kuliko kukariri wafundishwayo madarasani.

Ndiyo sababu, likawapo pia wazo la kuondokana na mitihani zaidi na badala yake kuzingatia majaribio ya mara kwa mara (continuous assessments), ilikufuatilia uwezo na umahiri wa mwanafunzi badala ya kukaririshiwa mitihani.

Likawapo pia wazo miongoni mwa mawazo lukuki, la kuhakikisha kila shule inakuwa na madarasa ya awali, ambamo mtoto wa miaka mitano atasoma kwa mwaka mmoja kabla ya kufikisha miaka sita ya kuanza darasa la kwanza.

Nasema mjadala kwenye kongamano hilo, ulikiwa mpana na wa kina, lakini wenye kuzingatia maslahi ya nchi na wananchi kwa ujumla wao. Watu walifunguka walichokuwa nacho, wakikiona cha maana kwao naTaifa lao.

Pamoja na mapendekezo hayo mengi yaliyotolewa na wahusika, kutaarifu kuwa yataendelea kuchakatwa hatimaye kufikishwa bungeni kutungiwa sheria, kuna lililoniacha hoi.

Nalo ni la Kiswahili kama lugha mahususi ya kufundishia shuleni, ambamo kuliibuka hoja mbili tofauti, za kuunga mkono na za kupingana kwa sababu mbalimbali tofauti, sambamba na la kutaka watu wajifunze Kireno na Kichina!

Nilishangaa na bado nashangaa, kwamba kuna Watanzania bado wanaona Kiingereza ndiyo lugha mwafaka ya kufundishia shuleni, eti ndiyo inaweza kutuunganisha na mataifa mengine.

Wanasahau kuwa kuna watu huko duniani wanatamani kujua Kiswahili na ndiyo sababu mpaka sasa kuna mataifa yameagiza walimu wa Kiswahili kutoka Tanzania kwenda kufundisha watu wao.

Wanashindwa kuelewa, kuwa ni Tanzania pekee barani Afrika, yenye lugha yake ya Taifa (Lingua Franca) ambayo si ya kigeni au si lugha za Wakoloni, kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno.

Ni kasumba tu iliyotujaa akilini, kuona kwamba Kiingereza ndicho kila kitu kwetu, tunasahau kuwa mataifa mengine ya kigeni ambako huko nyuma tulipeleka watu wetu kujifunza, yalitoa na yanatoa mafunzo kwa lugha zao.

Mtu akienda kusoma Ujerumani, Ufaransa, Uchina, Russia na kwingineko, kwanza alitakiwa au anatakiwa atumie muda kujifunza lugha za huko kabla ya kuanza mafunzo.

Lakini, sisi tunaendelea kukumbatia lugha za kigeni na ndiyo sababu mtu akishalewa pombe au bangi kidogotu, anasahau lugha ya mama yake na kuanza kutamba kwa Kiingereza, kama kipimo cha mtu aliyesoma au mwenye daraja la juu kiuchumi!

Kwenye Kongamano hilo, aliibuka raia wa kigeni kutoka Uswidi, Mia Mjengwa Bergdahl na kutuzodoa Watanzania, tunaokataa kutumia Kiswahili chetu kufunzia wanetu.

Akatoa mfano wa jinsi kwao Uswidi walivyotumia lugha yao kufundishia watu wao na kuwawezesha kuelewa vitu kirahisi sana, akisema kama ni kutafsiri misamiati mbona inawezekana!

Katika kuthibitisha hilo, Mia akatoa mfano jinsi walivyolazimishwa nchini kutumia mitaala ya VETA kwa Kiingereza, ambao wanafunzi hawakuwa wakielewa vizuri na matokeo yake wakafeli, lakini sasa baada ya kutumia Kiswahili ufaulu umepanda!

Watanzania tuache kusujudia vya kigeni na kuacha vyetu, kwa kutaka tu kuonekana tumesoma kwa kuzungumza Kiingereza, Kireno, Kifaransa na sasa tunaingia kwenye Kichina, tutaachwa! Mazingira yetu ni ya Kiswahili siKichina!

Kana kwamba haitoshi, tumekumbatia mpaka dini za kigeni na kuachana na za kiasili... Usiache mbachao kwa msala upitao. Alamsiki!

UCHUMI

## MARSHALL MBISE

# Mama mwenye ulemavu miaka 23 katika mapambano magumu kujikimu

**Na Devota Mwachang'a**

"Hujafa hujaumbika" ndio kauli inayomuangukia Marshall Mbise mkazi wa Kipunguni kwa Diwani, wilayani Ilala, mkoa wa Dar es Salaam. Ni mwanamke mzaliwa wa mwaka 1979 katika kijiji cha Mikunda wilayani Tandahimba, Mtwara.

Marshall anasema kayafurahia matumizi ya viungo vyake vyote kwa takribani miaka 20 ya maisha yake, hata kufikia siku akajikuta kagogwa na gari akiwa nje ya nyumbani kwao, kulikokuwa pembezoni mwa barabara itokayo Maundo kuelekea Newala, Mtwara.

Ni ajali iliyomsababishia ulemavu kuanzia uti wa mgongo hadi miguu, akinusurika mikono yake, hata ndio ikamuwezesha kuingia katika orodha ya wajasiriamali, akitengeneza batiki aina ya'tie & dye', anafuma maua kwenye shuka, foronya na vitambaa.

Mama huyo, Marshall pia ni mtaalamu wa kutengeneza bidhaa za shanga kama mikoba, mikufu, heleni, mapambo na nyingine kwa lengo la kupata pesa ya kujikimu na kulea familia yake.

**SAFARI YAKE**

"Nilipata elimu ya msingi katika Shule ya Msingi Mikunda Tandahimba mkoani Mtwara, kuanzia mwaka 1988 hadi 1994. Baada ya kumaliza darasa la saba mwaka uliofuata 1995 niliolewa na kujaliwa kupata mtoto wa kike.

Mimi na mume wangu na mtoto tuliendelea kuishi kwa furaha pale kijijini, kabla ya kupata ajali," anasimulia.

Marshall anasimulia mzizi wa mkasa anasema, kuna wakati akafungasha safari ya kwenda kumsalimia mama yake, pia ndugu, miezi kadhaa imepita tangu baba yake kufariki dunia.

Ilikuwa siku ya Jumamosi Desemba 11 mwaka 1999, akiwamo mtoto wa miaka mitatu wamesimama nje na ndipo magari mawili kwenye mwendo, yakaacha njia na kuwaparamia kabla ya kuserereka na kujikita kwenye nguzo ya nyumba.

Mbise anasema athari hiyo imemuachia alama ya kudumu kwenye maisha yake ikayabadilisha, akinena: "Mimi na kaka yangu tuligongwa na lile gari ila aliyeathirika sana ni mimi.

"Nilisimuliwa kuwa nilipoteza fahamu nikabebwa na kuingizwa kwenye gari lile lile lililohusika kwenye ajali hadi kituo cha Polisi Mahuta kupatiwa Fomu (PF 3).



Picha tofauti za maisha ya Marshall Mbise. **PICHA ZOTE: DEVOTA MWACHAN'GA.**

Kabla ya kupelekwa hospitali ya Newala, ambako nilirejewa na fahamu nikakaa siku nzima bila huduma ya dawa wala maji ya kunywa.

"Ndugu zangu hawakukubaliana na hali ile, wakabishana na wauguzi hatimae nikapelekwa Hospitali ya Ndanda Masasi huko nilifanyiwa vipimo na kugundulika kuwa Uti wa mgongo umepata madhara nikaanzishiwa matibabu." Mbise anaeleza kuwa kwa zaidi ya miezi mitano kuhudumiwa kitandani hospitali, madakatari walimweleza hatojiweza kwa mengi .

Anasema wiki mbili kabla ya kuruhusiwa kutoka Hospitali ya Ndanda, madaktari walimueleza ukweli mengi yakiwamo ya faragha za kibinadamu.

"Niliwaza kama nisingekuwa na mtoto ningeweza hata kujiua. Ila madaktari ni kama waliyasoma mawazo yangu wakanitia moyo na kuniambia hauna haja ya kujiua, kubali matokeo utaishi kama hao wazima wanavyoishi, usione aibu hata utakapochafuka kwa kutokwa na haja bila kujua," anasema.

Mnamo mwaka 2007, anasema akaenda kumsalimu bibi yake anayeishi kijiji cha Mkupete, alikokutana na kijana Mustapha Naheka aliyekuwa anaishi na ulemavu.

Huyo akamshawishi aende kwenye Chuo cha Walemavu cha Ufundi Stadi Yombo, mkoani Dar es Salaam kwa ajili ya kupata mafunzo kuboresha ujuzi wake wa kufuma.

"Mustapha alinipa mwongozo, nikaandika barua kuomba nafasi ya masomo Chuo cha Walemavu cha Ufundi Yombo, nikajibiwa. Januari 2008 nikaja Dar es Salaam, nilisindikizwa na mama yangu," anaeleza na kuendelea:

"Lakini pale chuoni hawakuruhusu mwanafunzi kuishi na ndugu. Hivyo, nililazimika kuishi maisha magumu sana ya kujitegemea kwa miaka miwili niliyosoma pale kuanzia Januari 20, mwaka 2008 nilipoanza mafunzo hadi 2009."

Marshall anasema, akiwa masomoni akapatwa na vidonda vilivyokuwa vinatoa wadudu, vilivyosababishwa na kukaa muda mrefu, pia akikosa muda wa kubadilisha nguo na kujisafisha baada ya kutokwa na haja.

Anasema, akapelekwa katika Hospitali ya Rufani Temeke na baadaye, akahamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili kwa matibabu ya kina.

**HATUA MPYA**

Hapo anasimulia maisha yake hospitalini Muhimbili akisema" "Nilikutana na Padri Fidelis Mushi wa Shirika la Wakamiliani Parokia ya Yohane wa Mungu Yombo Vituka, ambaye kwa wakati ule alikuwa Parokia ya Muhimbili. Kipindi kile akawa anafuatilia afya yangu akishauriana na madaktari hadi nikapona.

"Nilifanikiwa kumaliza mafunzo na baada ya pale, Padri Mushi akanipangishia chumba cha kuishi Mwananyamala Kinondoni, kisha kwa ushirikiano na wafadhili wengine alinipeleka Chuo cha Kompyuta pale Vijana Center (Ilala) nikajifunza na kupata cheti, sikuweza kupata ajira kutokana na miundombinu haikuwa rafiki kwa hali yangu."

Anaendelea: "Kwa msaada wa mama yangu niliyekuwa naishi naye, niliamua kuanza kufanya kazi za kufuma vitambaa, mashuka na batiki, japo nilikuwa nashona nguo kwa kutumia cherehani yangu ya mkono.

"Sikupenda kushona nguo za watu kwa sababu nilihofia watu kuja mara kwa mara ilhali mimi nahitaji faragha kutokana na tatizo la kutokwa haja bila kujua, nikaamua kuachana na ushonaji guo."

**MAISHA YAKE**

Marshall anasema, kwa sasa anaishi kwenye chumba kimoja na binti yake mwenye umri miaka 27, anayemsaidia kila hali, japo ana tizo la ugonjwa Kifafa, pia mtoto mdogo umri miaka mitatu.

Mama huyo anasimulia uhalisi wa maisha yao ni magumu, ikiwamo makazi yake hayampi nafasi ya kupata furaha kimaisha, akitanguliza ombi kwa umma kupata makazi yenye vyumba, ili yamsitiri, sasa akiishi kweye chumba kimoja, akielemewa hata na kodi.

Mama huyo anasema, katika kutengeneza bidhaa zake anakabiliana na changamoto ya kukosa soko la bidhaa hizo, pia mtaji wa kuendesha uzalishaji.

Anadokeza, mtoto wake (Yusta), ndiye anayesaidiana naye kutengeneza bidhaa kama mikoba, pia ndio anayepambana kutafuta masoko, akimuwakilisha mama yake.

Yusta ananena: "Kuna wakati tunapishana na fursa kutokana na kuishi huku mbali na zinakopatikana. Wakati mwingine niliwahi kupeleka bidhaa za mama kwenye maonyesho, ila ikawa ngumu yeye kufika.

"Hatukuwa na usafiri wa kutufikisha pale, pia tunakosa vifaa bora vya kutengenezea na kuboresha bidhaa zetu. Muda mwingi najishughulisha na biashara ndogondogo hapa mtaani ili tuweze kujikimu."

Kuhusu ndoa yake anafafanua: "Mume wangu alinitelekeza nikiwa hospitali baada ya miezi miwili tangu nipate ajali, ile hali yangu alionea kinyaa, ikafika wakati akawa hafiki hospitalini.

" Hata nilipotoka hospitali nikaenda pale kwangu tulipokuwa tunaishi pamoja akaondoka ndugu zangu walikutana nae mitaani, lakini hakujali ilifikia hatua nililazimika kuhama pale nikaambatana na mama yangu tukarudi nyumbani. Sijui alipo na wala hajawahi hata kututafuta kwa miaka hii zaidi ya ishirini," anasimulia Mbise.

- ***Kumsaidia Marshall Mbise, wasiliana na Padri Fidelis Mushi wa Kanisa Katoliki Parokia ya Yohane wa Mungu Yombo Vituka kupitia simu namba +255755513688 au Benki ya Mkombozi, mwenye akaunti Fidelis S. Mushi, namba ya akaunti 00121200770601.***





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, Dk. Selemani Jafo (kushoto), akijadiliana jambo na Waziri wa Mazingira, Kilimo na Mifugo wa nchi ya Burundi, Prof. Sunctus Niragira walipokutana katika viwanja vya Bunge, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Sarakasi ndani ya CWT zazidi kunoga

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

SAKATA la vurugu za Chama cha Walimu Tanzania (CWT) limeibua sura mpya baada ya baadhi ya viongozi wake wakiwamo wenyeviti wa mikoa kuibuka na kuiponda kamati ya utendaji kwa kumsimamisha Katibu Mkuu, Japhet Maganga.

Viongozi hao wamesema kitendo kilichofanywa na kamati hiyo ni uhuni kwa kuwa kinakinzana na katiba ya CWT.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti juzi, jijini hapa, baadhi ya viongozi hao walisema kitendo kilichofanywa na baadhi ya wajumbe wa kamati ya utendaji ya chama hicho kinakiuka katiba na kanuni za chama hicho.

Mwenyekiti mstaafu wa chama hicho Mkoa wa Dodoma, Clement Mahemba, alisema taratibu za chama zinaeleza wazi kwenye katiba ya CWT, tofauti na ambavyo wajumbe hao walivyochukua uamuzi uliovunja katiba ya chama.

Mahemba, alisema kama kuna mwanachama ambaye ana hoja yake, kuna njia sahihi za kufuatwa na si kama ambavyo wajumbe hao wamefanya.

"Kikao cha kamati tendaji kinazo taratibu rasmi na mialiko rasmi ya mwenyekiti lakini wamefanya uhuni wa kuendesha kikao chini ya mti na kuja na maazimio ambayo hayana msingi. Niwashauri kama wana jambo lao wasubiri vikao rasmi kwani kamati hii haina uwezo wa kumsimamisha katibu mkuu isipokuwa baraza kuu na baadaye ni mkutano mkuu wa chama," alisema Mahemba.

Pia aliwataka walimu nchini kuwa na imani na viongozi wao waliopo madarakani na kuacha kusikiliza magenge ya watu ambao wamekuwa na hoja binafsi zisizobeba maslahi ya wanachama kwa lengo la kukiyumbisha chama hicho.

James Ndyanabo, Mwenyekiti wa CWT Biharamulo, alisema taasisi hiyo inayo miongozo yake ambayo kila mwanachama anatakiwa kuifuata na si kila mtu kuja na uamuzi wake ambao unavunja katiba ya chama.

"Niwaombe walimu wote nchini kutoa ushirikiano kwa viongozi wetu wakati huu hadi hapo ambapo maamuzi mengine yatakapo tolewa na vikao vya juu ikiwemo baraza kuu pamoja na mkutano mkuu kuhusu sakata hili," alisema.

Hivi karibu, wajumbe 18 katika 32 wa kamati tendaji ya CWT walikutana jijini hapa na kufanya kikao ambacho kiliibuka na maazimio ya kumsimamisha Maganga kujihusisha na shughuli zozote za chama na nafasi hiyo kupewa naibu katibu mkuu.

# Waziri ataka elimu haki usalama wazee

**Na Renatha Msungu**, DODOMA

WAZIRI wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Dorothy Gwajima, amewaagiza wakuu wa mikoa nchini kutoa elimu ya kina kwa wananchi kuhusu haki, ulinzi, usalama na ustawi wa wazee.

Dk. Gwajima alisema hayo jana wakati akizungumza na wajumbe wa Baraza la Wazee Kata ya Mkonze, mkoani Dodoma ikiwa ni sehemu kuelekea maadhimisho ya Siku ya Kupinga Ukatili dhidi ya Wazee yatakayofanyika Juni 15, mwaka huu.

Waziri Gwajima alisema kutokana na kuboreshwa kwa huduma za kijamii nchini, idadi ya wazee imeongezeka kutoka 2,507,568 hadi 5,008,339 sawa na asilimia 8.1 ya Watanzania 61,741,120.

Kutokana na hali hiyo, alisema serikali imeendelea kuadhimisha siku ya kupinga Ukatili dhidi ya Wazee kila Juni 15 na maadhimisho haya ni muhimu kwa ajili ya kuuhabarisha umma juu ya haki, ulinzi, maendeleo na ustawi wa wazee nchini.

Aidha, alisema katika kulinda haki ya wazee kuishi, serikali imeendelea kutekeleza Mkakati wa Kitaifa wa Kutokomeza Mauaji kwa Wazee kwa sababu wana haki ya kuishi kama ilivyo jamii ya rika lingine. "Ninaomba wakuu wa mikoa yote nchini kuratibu maadhimisho haya kimkoa kwa kushirikiana na viongozi wa mabaraza ya wazee katika mikoa husika tunapoelekea kwenye maadhimisho hayo," alisema Dk. Gwajima.

Waziri Dk. Gwajima alisisitiza kuwa jamii inapaswa kuacha kufanya ukatili dhidi ya wazee na makundi yote kwa ujumla huku akiwaomba wanahabari kutumia kalamu zao kuelimisha na kuendelea kukemea masuala ya ukatili kwa wazee nchini kote.

"Serikali itaendelea kuchukua hatua stahiki kuwashughulikia ipasavyo wale wote watakaobainika kufanya vitendo vya ukatili kwa makundi mbalimbali katika jamii hususani kwa wazee," alisema.

Dk. Gwajima alisema hakuna sababu yoyote ya kuwanyanyasa wazee ikiwamo kuwafanyia ukatili kwa sababu na wao wanahaki ya kuishi kama ilivyo jamii nyingine inayotuzunguka katika maeneo mbalimbali hapa nchini.

Maadhimisho ya kupinga ukatili dhidi yaWazee mwaka huu yatafanyika katika ngazi ya mikoa kote nchini na kaulimbiu ni "Wazee Wanastahili Heshima na Usikivu Wetu".

# Machifu waapa kulinda maadili

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MACHIFU wa mkoa wa Dodoma wamesema wataendelea kushirikiana na serikali katika kulinda maadili mema kwa jamii inayowazunguka kwenye maeneo yao ikiwemo kukemea vitendo viovu vinavyojitokeza hivi sasa nchini.

Mlezi wa Machifu Mkoa wa Dodoma, Mohamed Keba, alisema hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa kwenye kikao cha Kamati ya Utendaji ya Machifu ya Mkoa wa Dodoma kwa ajili maandalizi ya tamasha la utamaduni litakalofanyika Septemba, 2023 jijini hapa.

Alisema machifu watashirikiana kikamilifu na serikali katika uboreshaji wa maadili pamoja na kukemea vitendo viovu vinavyojitokeza kwa jamii na kwenye shughuli mbalimbali za kimaendeleo.

Alisema machifu hao watahakikisha wanahamasisha katika kutatua migogoro mbalimbali ikiwemo ya ardhi ili kuimarisha mahusiano mema maendeleo kati yao na jamii na serikali kwa faida ya watanzania bila kujali itikadi yoyote.

Keba ambaye pia ni Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi Kata ya Ipagala mkoani Dodoma, aliiomba jamii kuwaamini, kuwasikiliza na kushirikiana na machifu kutokana na mchango wa shughuli za kimaendeleo yanayofanywa ikiwemo kutatua migogoro.

"Machifu wana uwezo wa kuhamasisha jamii katika masuala ya maendeleo kwenye maeneo yao,hivyo wanatakiwa kuaminiwa,kushirikiana na kusikilizwa kwa lengo la kuleta maendeleo kwa upande wa jamii yote," alisema.

Mwenyekiti wa Machifu Mkoa wa Dodoma, Mtemi Bilinje Ally, aliwataka kushirikiana kwa ukamilifu katika kuanzisha vitalu vya kuotesha miche ya miti kama serikali inavyoagiza ili kuufanya mkoa wa Dodoma kuwa ya kijani.

Mtemi Bilenje, aliwataka machifu hao kila mmoja kwenye maeneo yake kuiunga mkono serikali kutokana na juhudi kubwa zinazofanywa ikiwamo kuhimiza uanzishaji wa vitalu vya miche kupanda na utunzaji wa miti kwenye maeneo mbalimbali.





Ofisa Elimu Vifaa na Takwimu wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Fabian Mtisi (katikati), akitoa elimu ya usafi kwa wanafunzi wa Shule ya Msingi Lupeta, kata ya Swaya Halmashauri, baada ya kuwekewa mfumo wa maji na kujengewa vyoo vya kisasa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kupitia mradi wa SAWA. **PICHA: NEBART MSOKWA.**

# Halmashauri yavunja mkataba na TBA

**Na Grace Mwakalinga,**
KYELA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kyela mkoani Mbeya, imevunja mkataba na Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) katika usimamizi wa jengo la wadi ya mama na mtoto katika hospitali ya wilaya hiyo.

Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Katule Kingamkono, alithibitisha hayo jana alipozungumza na Nipashe baada ya kuwapo kwa tetesi kuhusu kuvunja mkataba na TBA kutokana na kusuasua kwa ujenzi wa jengo hilo.

"Kupitia vikao vyetu vya kawaida tulipokea taarifa kuwa tayari mkataba umevunjwa kwa sababu kasi ya TBA katika ujenzi huo, ilikuwa ya kusuasua, hivyo basi kazi iliyobakia itakuwa chini ya halmashauri kwa kushirikiana na wataalam ambao watahakikisha wanakamilisha kwa wakati na wananchi kuanza kupata huduma za matibabu," alisema Kingamkono.

Kuhusu fedha zilizotolewa na serikali kuu kwa ajili ya mradi huo kurudishwa baada ya kuvunjwa kwa mkataba, Kingamkono alisema Desemba, 2022 walipokea Sh. milioni 750 na kwamba hadi wanavunja mkataba zilikuwa zimebaki Sh. milioni 600 hivyo watafanya mawasiliano na serikali kuu kuwajulisha suala hilo na kuandika barua ya kuomba fedha hizo ili ziendelee kutumika katika mradi huo.

Mei 2, mwaka huu, Baraza la Madiwani lilimwagiza Mkurugenzi wake, Ezekiel Magehema, kuvunja mkataba na TBA endapo ataendelea kusuasua kukamilisha ujenzi wa wadi hiyo.

Alisema baraza lilifikia uamuzi huo baada ya kuona kasi ya ujenzi hairidhishi licha ya serikali kutoa fedha nyingi kwa ajili ya kukamilisha mradi huo ambao utakuwa mkombozi kwa kina mama na watoto wilayani humo.

Tumaini Mwakatika, Diwani wa Viti Maalum, alisema wameridia kuvunja mkataba huo na kumtafuta mtu mwingine ambaye ataukamilisha kwa ajili ya kuanza kutolewa huduma za matibabu kwa wajawazito na Watoto.

"Ni kweli katika kikao cha baraza la madiwani cha robo ya tatu tulikuwa na majadiliano kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa jengo la wadi ya mama na mtoto katika hospitali ya wilaya ya Kyela.

Tulimtaka mkurugenzi kuzungumza na fundi mkuu katika mradi huu ambaye ni TBA kujua ni lini atakamilisha.

Ujenzi wa wadi ya mama na mtoto katika hospitali ya wilaya ya Kyela ulianza mwaka 2021 baada ya jengo lililokuwapo kuungua na majengo mengine kuchakaa. Serikali ilitoa Sh. bilioni 2 kwa ajili ya kukamilisha ujenzi huo huku wadau nao wakitoa michango yao na tulikata ujenzi huo ukamilike mwaka 2022 lakini imekuwa tofauti.

# Madiwani watwishwa zigo mapato ya ndani

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya, Bosco Mwanginde, amewataka madiwani wa halmashauri hiyo kusimamia ukusanyaji wa mapato kama sehemu ya utekelezaji wa majukumu na kuisaidia serikali kuongeza mapato.

Mwanginde alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao cha baraza la madiwani huku akisema ni muhimu suala la ukusanyaji mapato likatiliwa mkazo kwa sababu wilaya hiyo kwa sasa ina idadi kubwa ya watu kutokana na shughuli za uchimbaji wa dhahabu na kilimo cha tumbaku.

"Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, wilaya ya Chunya ina ongezeko la watu kwa asilimia 120 ukilinganisha na idadi ya watu kwa mujibu wa sensa ya mwaka 2012 sasa kuna watu 344,471," alisema.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Simon Mayeka, alikemea tabia za watoza ushuru ambao huwatoza wafanyabiashara na wakulima fedha ambazo ziko nje ya utaratibu akisema kufanya hivyo ni kinyume cha sheria za nchi na ni kosa la uhujumu uchumi.

Alisema Jeshi la Polisi litamshughulikia mtoza ushuru yeyote atakayebainika kumtoza mwananchi fedha ambayo ipo kinyume na utaratibu.

"Tunaomba Jeshi la Polisi lianze kuwakamata mawakala wote wanaowatoza fedha wananchi ikiwemo huduma ya kutuma fedha jambo ambalo ni kinyume na utaratibu," alisema.

Mayeka alitoa maagizo hayo baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa madiwani kwamba kuna mawakala wa fedha wanamtaka mwananchi kutoa kiasi cha Sh. 500 ili kuwekewa fedha kuanzia Sh. 10,000.

# Wakulima wataka elimu matumizi chokaa

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAKULIMA wa mazao mchanganyiko mkoani Mbeya, wameiomba Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, kutoa elimu ya matumizi sahihi ya chokaa baada ya kubaini ina uwezo mkubwa wa kudhibiti tindikali ardhini.

Ombi hilo limetolewa baada ya TARI Uyole kutoa taarifa ya asilimia 14 ya ardhi inayotumika kwa kilimo Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kuathirika na tindikali na kubaini chokaa kuwa mwarobaini wa kukabiliana nayo.

Wakizungumza na Nipashe kwa nyakati tofauti, walisema wameshtushwa na takwimu hizo na kuomba serikali kupitia TARI kuanza kutoa elimu ya matumizi ya chokaa kabla ya msimu mwingine wa kilimo kufika.

Witness John alisema kutokana na madhara hayo, kuna kila sababu hatua zichukuliwe mapema kwa wataalam wa kilimo kuwafikia kutoa elimu ili waweze kuthibiti tindikali iliyoathiri ardhi .

Rachel Fredy alisema ni wakati sasa serikali kuwekeza nguvu kwenye kilimo cha mazao ya chakula na biashara ikiwepo upatikanaji wa mbolea,viwatilifu kwa wakati sambamba na maofisa kilimo kuwafikia.

"Madhara haya ya udongo yanatokana na wakulima kukosa elimu ya kukabiliana na matumizi ya kemikali kwenye udongo kutokana na maofisa kilimo kutotekeleza majukumu yao kwa wakati.

Tunahitaji msaada katika hili ili madhara yasiwe makubwa zaidi na kusababisha mazao kuharibika shambani," alisema Recho.

Mtafiti wa Afya ya Udongo TARI - Uyole, Fredrick Mlowe, alisema asilimia 14 ya ardhi katika mikoa ya Nyanda za Juu Kusini imeathirika na tindikali.

"Utafiti unaonyesha kati ya ekari moja ya mazao mkulima anastahili kuvuna tani tatu na zaidi lakini hali imekuwa tofauti kutokana na mazao kushindwa kufyonza mbolea inayowekwa kutokana na madhara ya tindikali "alisema Mlowe.

Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni ya Saruji mbeya, Khaled Ghareob, alisema wamepokea ombi hilo la serikali na watahakikisha wanazalisha chokaa ya kutosha na kuisambaza kwa wakulima kulingana na mahitaji ili kusaidia ardhi ya kilimo isiathirike zaidi.



## HABARI ZANZIBAR

# Wizara yakiri uwapo kemikali zisizofaa maabara za shuleni

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekiri kuwapo kemikali nyingi katika maabara za shule za Unguja na Pemba ambazo zimepitwa na wakati, hivyo zinahitaji kuteketezwa ili kuepuka kusababisha athari zaidi kwa wanafunzi.

Hayo yalisemwa jana katika Baraza la Wawakilishi na Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Abdulgulam Hussein, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Ziwani (CCM), Suleiman Makame Ali. Mwakilisho huyo alitaka kujua lini wizara itazipatia ufumbuzi kemikali zilizoko katika shule mbalimbali ambazo tayari zimepitwa na wakati na kutishia afya za wanafunzi.

Naibu Waziri alisema wizara tayari imeanza kufanya tathmini ikiwamo kuziorodhesha shule zote ambazo kemikali zinazotumiwa na wanafunzi kwa ajili ya kazi za vitendo vya masomo kuona zinaharibiwa.

Alizitaja kemikali hizo ni zile zinazotumika kwa ajili ya masomo ya vitendo ya Kemia na Baiolojia ambavyo muda wake unapopita zinaweza kusababisha madhara makubwa.

Katika kuziharibu kemikali hizo, alisema ushirikiano zaidi unahitajika na kufanya kazi kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali ikiwamo Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Alisema Ofisi ya Mkemia Mkuu ndiyo inayoshughulikia masuala ya maabara za kemikali mbalimbali na kwamba ushiriki wake unahitajika ikiwamo kutoa ushauri wa kitaalamu.

Kwa mujibu wa Naibu Waziri, baadhi ya kemikali ambazo zimekaa muda mrefu tayari zimeanza kuleta athari katika shule hivyo uondoshaji wa kemikali hizo ni muhimu.

"Mheshimiwa Spika naomba kukiri kwamba shule nyingi kemikali zake katika maabara zimepitwa na wakati kwa hivyo tumejipanga kuziharibu kwa njia mbalimbali ili kuwafanya wanafunzi wetu kuwa salama," alisema.




Kiongozi wa Umoja wa Mataifa Zanzibar, Dorothy Temu Usiri akizungumza na waandishi wa habari, baada ya mkutano wa mfumo wa uratibu wa ahadi ya mawaziri kuboresha elimu na afya kwa vijana wa nchi za Mashariki na Kusini mwa jangwa la Sahara, uliofadhiliwa na shirika la maendeleo la Sweden (SIDA), kisiwani humo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Katibu Mkuu asisitiza umuhimu malezi bora kwa vijana na watoto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Omar Dadi Shajak, amesisitiza umuhimu wa malezi bora kwa watoto na vijana kwa kuwa ndio hazina ya taifa lolote duniani.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano wa Mfumo wa Uratibu wa Ahadi ya Mawaziri Kuboresha Elimu na Afya kwa Vijana wa nchi za kusini mwa jangwa la Sahara uliofanyika visiwani Zanzibar. Mkutano huo umefadhiliwa na Shirika la Maendeleo la Sweden (SIDA).

Alisema katika nchi za mashariki na kusini mwa Afrika idadi ya vijana wa miaka 10 hadi 24 inakisiwa kufikia milioni 158 ikiwa ni sawa na theluthi moja ya idadi ya watu katika maeneo hayo. Kwa muktadha huo, alisema kuna haja ya vijana hao kuwekewa mazingira ya kustawisha afya na maisha yao kwa ujumla ili kukabiliana na maisha ya sasa na baadae kuleta maendeleo ya nchi.

Dk. Shajak alisema katika miaka ya hivi karibuni, kumekuwa na msukumo mkubwa duniani kote katika jitihada za kuongeza huduma kamilifu za afya ya uzazi na elimu ya jinsia kwa vijana.

Alisema hali hiyo imetokana na kuongezeka kwa mimba za mapema, vitendo vya udhalilishaji na maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi kwa makundi hayo.

"Kutokana na changamoto hizi nchi za mashariki na kusini mwa Afrika zipatazo 20 ikiwamo Tanzania, ziliamua kupitisha na kuweka maazimio ya pamoja kuanzia mwaka 2013 hadi 2020 na utekelezaji wake utapunguza changamoto hizo," alisema Dk. Shajak.

Alisema maazimio hayo ambayo yamewekewa muda na shabaha maalum na utekelezaji wake umesaidia kupunguza changamoto lakini shabaha hazikuweza kufikiwa kwa sababu kundi hilo linaendelea kuathirika kwa matatizo hayo.

Pia alisema maambukizi ya virusi vya Ukimwi yalitakiwa kupunguzwa kwa asilimia 90 na mimba za mapema kwa asilimia 75 ifikapo mwaka 2020.

Kiongozi wa Umoja wa Mataifa (UN) Zanzibar, Dorothy Temu, alisema umoja huo unafuatilia maendeleo ya vijana na watoto hasa katika elimu na afya na kwamba changamoto kubwa sasa iko katika afya ya uzazi, udhalilishaji, ajira kwa vijana na maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Alisema lengo la mkutano huo ni kujadili maeneo hayo ili kuleta mabadiliko katika nyanja hizo ikiwemo suala la afya ya uzazi ili kuokoa maisha ya vijana na watoto.

Washiriki wa mkutano huo, walisema kuna haja ya kufanyika kwa tathmini ya miaka iliyopita kuhusu masuala ya udhalilishaji, afya, elimu, ajira ili kujua muelekeo wake miaka ijayo.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, kwa mwaka 2022 matukio 1,360 ya udhalilishaji wa kijinsia yaliripotiwa katika vituo vya polisi Unguja na Pemba.

Mkutano huo umeweka mpango kazi wa nchi kwa wadau wa elimu, afya na vijana ili kuboresha upatikanaji wa takwimu za utekelezaji wa maazimio hayo na kuandaa ripoti ya kitaifa kila mwisho wa mwaka.

# Mke wa Rais ageukia usalama wa chakula

**Na Mwandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Taasisi ya Zanzibar Maisha Bora (ZMBF), Mama Mariam Mwinyi, ameitaka jamii kuzingatia suala la usalama wa chakula ili kujikinga na maradhi yatokanayo na chakula kisicho salama.

Mama Mariam ambaye pia ni mke wa Rais wa Zanzibar, aliyasema hayo kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Usalama wa Chakula yaliyofanyika viwanja vya Mwembe Kisonge, Wilaya ya Mjini Unguja.

Alisema kuna ongezeko la maradhi yanayosababishwa na usalama mdogo wa chakula, jambo alilosema linaathiri afya kwenye jamii.

Alitaka jamii kula vyakula salama kwa kufuata mtindo mzuri wa kula pamoja na kufanya mazoezi ili kuipunguzia Serikali mzigo mkubwa wa matibabu.

Mwenyekiti huyo ZMBF alisema moja ya malengo ya kuanzishwa kwa taasisi hiyo ni kuona namna bora ya kuunga mkono jitihada za kitaifa na kimataifa kwenye suala zima la kuimarisha lishe, afya na ustawi wa Wazanzibari ili kukuza maendeleo ya kiuchumi husussan kwa wanawake, watoto na vijana.

Alisema Siku ya Usalama wa Chakula Duniani ni jambo jema linaloleta uelewa mpana juu ya mambo yanayohusu usafi na usalama wa chakula katika kupunguza maradhi na kuimarisha uchumi wa Zanzibar.

Kutokana na umuhimu huo, aliwasihi watunga sera, Mamlaka ya Usalama wa Chakula, wanasayansi, wakulima, wauzaji wa chakula, wapishi, walimu, wanafunzi na watumiaji, kuongeza bidii za pamoja ili kuhakikisha mwamko wa usalama wa chakula unaongezeka Zanzibar.

Mama Mariam pia aliwataka watunga sera na waratibu kuhakikisha wanazingatia sera za udhibiti wa mifumo kwa usalama wa chakula na kuimarisha ushirikiano kwa wadau wote na kuhakikisha wanaifahamu miongozo na kuitumia mifumo iliyopo katika juhudi za kumlinda mlaji.

Alisema suala la usalama wa chakula ni pamoja na kuzingatia kula mlo uliotimia ili kupata lishe bora zaidi kwa watoto, wazee na wajawazito kwa kuimarisha mfumo wa kinga ulio imara na makuzi mazuri kwa watoto.

"Tujitahidi kula chakula kilicho safi kwa kuzingatia virutubisho na wingi unaofaa au unaohitajika". Alisisitiza.

Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema wizara kupitia taasisi zake inaweka taratibu bora za kudhibiti vyakula vibovu visiingie nchini.

"Tuhakikishe tunakula vyakula bora, usafi wa mazingira na uzalishaji wake, kwa bidhaa zote za mashambani na kwenye mifugo," alisisitiza na kuitaka jamii kufuata taratibu za kuvuna mara baada ya umwagiliaji na kupigwa dawa kwa mazao na wanyama.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTELEWA NA CHETI



**CHACHA M. HEGERA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.3634-0103 kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **MUGUMU SEKONDARI** mwaka 2012. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **SHY/RB/529/2017.**

## KUPOTELEWA NA CHETI



**MOHAMEDI RAMADHANI GWANDO** anatangaza kupotelewa na cheti cha Ualimu chenye index namba **E0523 - 0304** kilichotolewa na **MONDULI TEACHERS COLLEGE** mwaka **2018.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi: **ARU/KAR/RB/15611/2023.**

## KUPOTELEWA KWA KADI PIKIPIKI

**Abas Christopher Shumbu** anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki aina ya **SINORAY** yenye namba za usajili **MC. 799 DQL.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Abas kwa simu namba **0754972553.**

**Taarifa ya Polisi**
**SHI/SHI/RB/192750/2023.**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO WILAYA YA BUKOBA**
**KITUO CHA KALABAGAINE**
**SHAURI LA MADAI NO; 19/2023**
**BENEZETH SEVELIAN KAMKURU————————MDAI**
**DHIDI YA**
**TUMSIFU POSTA KYANDO——————————MDAIWA**

Tumsifu Posta Kyando unatakiwa kuhudhuria katika mahakama hii tarehe 28/06/2023 saa o8:30 hrs asubuhi kuja kujibu madai ukiwa na mashahidi wako.
Kwa kuwa ni siku ya kukata shauri fika na hati zote zinazohusiana na shauri hili na kama hautahudhuria shauri hili litaendelea kusikilizwa upande mmoja.
Hati hii imetolewa kwa amri yangu na mhuri wa Mahakama hii leo tarehe 01, June 2023.

C. R. RICHARD
HAKIMU MFAWIDHI
MAHAKAMA YA MWANZO KARABAGAINE.

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 63 of 2023**
**In the matter of the late STANLEY WILLISON NGALYA of Nala within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by MARIA HELEKO MOGWA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn. 369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 04 day of July........... 2023
Dated at Dodoma this 31 day of 05........2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**Probate and Administration Cause No 57 of 2023**
**In the matter of the late JOHN ZAKALIA CHIMBWI of Makulu within Dodoma City**
**And**
**In the matter of application for letters of administration by TUMAINI VALESI KAMBONA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 28 day of 06..........2023
Dated at Dodoma this 22 day of 05........2023

RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya DODOMA MJINI**
**Kituo cha DODOMA Mkoa DODOMA**
**Shauri la Madai/Ndoa Na. 56/2023**
**JINA LA MDAI........................THOMAS BEDA HYRA**
**JINA LA MDAIWA..................GRACE MAGUBO KAGORO**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya kanuni za taratibu Madai katika Mahakaka za Mwanzo)**

**KWA; GRACE MAGUBO KAGORO**
**Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba**
**MADAI YA TALAKA**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe **13/06/2023 saa 8:00** asubuhi/mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta Shahidi/Mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.
**ANGALIZO** kama hautohudhuria siku ilitajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 31/05/2023

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI**
**IDARA YA UHAMIAJI**



Hii ni Taarifa kuwa: **Bw. WADHAH ABDULQAWI QASEM** mwenye picha iliyoambatanishwa anaomba uraia wa Tanzania kwa mheshimiwa **WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** yeye anatokea nchi ya yemen na ni raia wa yemen. **Ndugu WADHAH ABDULQAWI QASEM** anafanya kazi katika kampuni ya **SHAFA AGRO LIMITED** Iliopo katika kijiji cha Nzihi kata ya Kidamali wilaya ya Iringa mkoa wa Iringa na alieingia nchini mwaka 2011. Kama kutakua na mtu yeyote mwenye pingamizi au sababu yeyote ya kupinga muombaji huyu asipewe uraia, atume taarifa yake kwa maandishi iliyosainiwa kwa **KAMISHNA JENERALI WA UHAMIAJI, S.L.P 1181, DODOMA.**

---

**ANDLUCKSTAR CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLY CO. LIMITED**
**P. O. BOX 859**
**MWANZA**

**RE: EXTRACT FROM MEMBERSRESOLUTION OF ANDLUCKSTAR CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLY COMPANY LIMITED HELD ON 23-05-2023 AT ITS OFFICE IN MWANZA**
**MIN: ACGS/BREALA/2023/001:**
**VOLUNTARY WINDING UP OF THE COMPANY**

At the meeting of the Members Resolution of the company held on 23-05-2023 at the office of the company in Mwanza, Members of the Company enormously resolved to voluntarily winding up the Andluckstar Construction & General Company Limited.
This resolution reads;
"The Chairperson asked the Members of the company to approve voluntary winding up of Andluckstar Construction & General Supply Company Limited".
All members agreed and approved the winding up of the company and it was further aghreed that company secretary was vested with authority to sign for this application to BRELA. BY ORDER OF THE MEMBERS

**Name: Andrea Benedict Massawe**
**Name: Frank Goodluck Mosha**

Signature: ...............................
**Chairperson**

Signature:...............................
**Secretary**

ANDLUCKSTAR CONSTRUCTION & GENERAL SUPPLY CO. LIMITED P.O. Box 859, MWANZA

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA TARIME**
**WILAYA YA TARIME**
**SHAURI LA RUFAA YA TALAKA NA. 03 YA 2023**
**PHILLIP NYANCHINI MOGENDI.............MUOMBA RUFAA**
**DHIDI YA**
**MONICA ANICET MAGUTU.............MJIBU RUFAA**
**MADAI YA TALAKA**
**KWA: MONICA ANICET MAGUTU**
**P.O.BOX 32 TARIME**

UNAFAHAMISHWA KWAMBA MLETA MAOMBI HAPO JUU AMEFUNGUA SHAURI LA RUFAA DHIDI YAKO KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA TARIME KWA MADAI YA TALAKA.

UNAAMRIWA NA MAHAKAMA HII: UHUDHURIE MBELE YA MAHAKAMA HII TAREHE 22/06/2023 SAA 02:30 ASUBUHI BILA KUKOSA KATIKA SHAURI LILILOTAJWA HAPO JUU NA NILAZIMA KULETA HATI ZOTE ZINAZOHUSU SHAURI HILO KWA AJILI YA KUJITETEA KATIKA SHAURI HILO.

ZINGATIA KWAMBA KUTOKUFIKA KWAKO TAREHE HIYO, SHAURI LITAANZA KUSIKLIZWA BILA WEWE KUTAARIFIWA TENA, NA MAAMUZI KUTOLEWA.

IMETOLEWA NAMI KWA AMRI NA CHAPA YA MAHAKAMA LEO TAREHE 02/06/2023

**HAKIMU WA WILAYA**
**MAHAKAMA YA WILAYA YA TARIME**
**TARIME**

---

**FOMU MIRATHI - 2**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya TEMEKE**
**Kituo cha JUMUISHI Mkoa DAR ES SALAAM**
**Usimamizi wa Mirathi Na. 838/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU KOMBO OMARY KIVUGO WA MUHEZA**
**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOTOLEWA NA OMARY HASSAN MLINDA**
**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 30 Mwezi 06 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kama yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 07 Mwezi wa 06 Mwaka 2023.

*OFISI ZA MATANGAZO*
*Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.*
*Mobile: +255 - 745 700 710.*
*E-mail: advertise@guardian.co.tz,*
*Website: www.ippmedia.com*

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
MOB: +255 - 0677020701
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ,
WEBSITE: WWW.IPPMEDIA.COM

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Samia kuongoza kikao cha Baraza la Taifa la Biashara

Na Mary Geofrey

RAIS Samia Suluhu Hassan, anatarajiwa kuongoza Kikao cha 14 cha Baraza la Taifa la Biashara (TNBC) kitakachofanyika leo, Ikulu jijini Dar es Salam.

Katibu Mtendaji wa TNBC, Dk. Godwill Wanga, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya mkutano wa 14 wa TNBC, yameshakamilika na wajumbe wa mkutano huo wamewasili Dar es Salaam.

Alisema kaulimbiu ya mkutano huo ni 'Mazingira Bora ya Biashara kwa Uchumi Himilivu na Shirikishi'.

Dk. Wanga alitaja moja ya mambo makubwa yatakayojadiliwa katika mkutano huo ni kupitia utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara (MKUMBI) au nchini ambapo wajumbe watapata fursa ya kujadili mafanikio, changamoto na mapendekezo ya maboresho ya utekelezaji wake.

Alisema mkutano huo pia utaeleza jinsi serikali inavyoshirikiana na sekta binafsi katika kuimarisha nchi kiuchumi.

Dk. Wanga alisema wajumbe wa TNBC pia watapata nafasi ya kupitia ripoti za utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa katika mkutano wa 13 wa TNBC ambao ulifanyika jijini Dodoma Juni 7 mwaka 2022.

"TNBC chini ya uwenyekiti wake, Dk. Samia, TNBC imepata mafanikio makubwa ikiwamo kuimarika kwa mahusiano na kuaminiana baina ya sekta za umma na binafsi sambamba na kufunguka na kuimarika kwa nchi kibiashara na uwekezaji," alisema.

Alisema mazingira ya biashara na uwekezaji yameendelea kuboreshwa nchini. Vikwazo vingi vya kufanya biashara na uwekezaji vimeondelewa, kwa sababu serikali inaaminiwa na wafanyabiashara na wawekezaji ndani na nje ya nchi.

"Mabaraza ya Biashara ya Wizara, Mikoa na Wilaya yaani MPPDs, RBCs na DBCs yamekuwa chachu kubwa ya kuibua fursa za kibiashara na uwekezaji katika uchumi wetu. Kupitia mabaraza hayo kero, tozo na makato mbalimbali yaliyokwaza biashara na uwekezaji zimetatuliwa," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, akizungumza katika mkutano na viongozi wa dini, mkoani humo jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tanzania na Burundi zakubaliana kulinda rasilimali Ziwa Tanganyika

**Na Robert Hokororo, DODOMA**

TANZANIA na Burundi zimekubaliana kuendeleza ushirikiano katika kulinda rasilimali zilizopo Ziwa Tanganyika ili kuleta manufaa ya kijamii na kiuchumi baina ya mataifa hayo mawili.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo alitangaza hatua hiyo jana baada ya kumalizika kwa kikao kati yake na Waziri wa Mazingira, Kilimo na Mifugo wa Serikali ya Jamhuri ya Burundi, Prof. Sanctus Niragira kilichofanyika jijini Dodoma.

Dk. Jafo alimhakikishia Prof. Niragira kuwa Serikali ya Tanzania kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais itahakikisha inasimamia kikamilifu Mkataba wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika ili kuhakikisha rasilimali zilizomo zinaleta tija na manufaa kwa wananchi wa nchi hizo mbili.

"Ninamshukuru Waziri mwenzangu wa Burundi kwa kuja nchini kwetu na kuona namna bora matumizi na usimamizi wa Ziwa Tanganyika ambalo linaunganisha mataifa yetu na wananchi wetu.

"Kikao kimewakutanisha wataalamu kutoka nchi zetu na kwa pamoja tumejadiliana na kubadilishana uzoefu wa namna ya kuhifadhi mazingira ya ziwa letu," alisema Dk. Jafo.

Pia alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuimarisha diplomasia katika ya nchi, hatua aliyoitaja kusaidia kuimarisha usimamizi endelevu wa rasilimali zikiwamo za mabonde ya mito, bahari na maziwa likiwamo Ziwa Tanganyika.

Aliitaja ni hatua inayozidi kuimarisha ushirikiano na mshikamano ya baina ya Tanzania na Burundi.

Waziri Niragira aliishukuru Tanzania kwa mwaliko huo kwa Serikali ya Burundi ambao umeleta tija katika namna ya kusimamia rasilimali za maji ikiwamo Ziwa Tanganyika ambalo linaunganisha nchi hizo mbili.

Alisema uhusiano wa nchi hizi mbili umezidi kuimarika baada ya kutiwa saini Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika Desemba 16, 2021 mkoani Kigoma ambao umekuza mipango ya maendeleo endelevu ikijumuisha uboreshaji wa miundombinu ya kimsingi, ufadhili wa maendeleo ya ndani na usimamizi shirikishi kupitia miradi tofauti.

Prof. Niragira ambaye pia ni Mwenyekiti wa Mawaziri wa Nchi Wanachama wa Mkataba wa Usimamizi Endelevu wa Ziwa Tanganyika, alisema nchi yake itaendelea ksuhirikiana na Tanzania katika kusimamia rasilimali za za Ziwa Tanganyika kwa manufaa ya wananchi wa mataifa hayo mawili.

Kikao hicho kilihudhuriwa na Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais, Mary Maganga, Naibu Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano), Abdallah Hassan Mitawi, Mkurugenzi Mtendaji wa Bonde la Ziwa Tanganyika, Tusanga Mukanga Sylvain, watendaji wa ofisi hiyo na watendaji wa wizara za kisekta.

Tanzania ikiwa ni miongoni mwa nchi wanachama imeendelea kushiriki kikamilifu katika shughuli zote zinazolenga kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za Ziwa Tanganyika ikiwa ni pamoja na utekelezaji wa programu za kikanda zinazolenga kulinda rasilimali za maji na ziwa hilo.

## CRDB yazindua kampeni akiba kwa ajili ya watoto

**Na Mwandishi Wetu**

KUELEKEA Siku ya Mtoto wa Afrika mwaka huu, Benki ya CRDB imezindua promosheni ya 'Timiza Ndoto Yake na Junior Jumbo' ikiwa na lengo la kuwahamasisha wazazi na walezi kuhusu umuhimu wa kuwawekea watoto wao akiba.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jijini Dar es Salaa jana, Meneja Mwandamizi wa Mauzo, Muhumuliza Buberwa, alisema kupitia kampeni hiyo benki pia imejipanga kutoa elimu ya fedha kwa watoto ili kuanza kuwaandaa mapema kukabiliana na changamoto za kifedha.

"Tumekuwa tukiwafundisha watoto juu ya mambo mbalimbali katika maisha, lakini watoto walio wengi wanakosa elimu kuhusu fedha na kujiwekea akiba, elimu ambayo ni muhimu sana kwa watoto na vijana wetu.

"Kampeni hii inakwenda kuhimiza juu ya ya umuhimu wa elimu pamoja na kuwafundisha watoto kujenga utamaduni wa kuanza kujiwekea akiba," alisema Buberwa.

Akielezea kuhusu muda wa kampeni hiyo, Meneja Mauzo wa Benki ya CRDB, Amina Mawona, alisema katika promosheni hiyo ya 'Timiza Ndoto Yake na Junior Jumbo, ambayo inatarajiwa kufikia kikomo Julai 5 mwaka huu, benki imetenga Sh. milioni 15.4 kama zawadi ya ada kwa ajili ya watoto 21 ambapo kila kanda ya benki hiyo kunatarajiwa kuwa na washindi watatu.

"Mshindi wa kwanza katika kila kanda atajishindia Sh. milioni moja, mshindi wa pili Sh. 700,000 na mshindi wa tatu Sh. 500,000, hivyo kufanya jumla ya zawadi za Sh. milioni 15.4. Lengo la promosheni hii ni kuhamasisha wazazi kujenga utamaduni wa kuwawekea akiba watoto," alisema.

Kushiriki katika promosheni hiyo, mzazi/ mlezi anatakiwa awe amefungulia akaunti ya 'Junior Jumbo' mtoto wake na kumwekea akiba mara kwa mara au kumfundisha kuweka akiba mwenyewe. Mzazi anaweza kuweka fedha katika akaunti ya Junior Jumbo ya mtoto kwa kutembelea tawi, kwa CRDB Wakala, kwa kuhamisha fedha kutoka akaunti yake kupitia SimBanking au Internet banking au kutoka mitandao ya simu.

Meneja wa Benki ya CRDB Tawi la Buza, Mary Joshua alisema wazazi wengi wamekuwa wakipata changamoto katika kulipa ada za watoto kutokana na wengi kutokuwa na utamaduni wa kuweka akiba kwa ajili ya watoto.

Hali hiyo imepelekea watoto wengi kuchelewa kurudi shuleni kuendelea na masomo au kujiunga na shule kwa wanafunzi wapya kutokana na kukosa mahitaji ya msingi ikiwamo ada.

"Tuna wahimiza wazazi/ walezi kuwafungulia watoto akaunti ya Junior Jumbo na kuanza kuweka akiba kwa ajili ya watoto kidogo kidogo. Akaunti hii inafunguliwa kwa vigezo nafuu sana, haina makato yoyote na hutoa faida ya riba kwa mteja," alisema Mary Joshua huku akisisitiza kuwa Benki ya CRDB imejipanga kutoa elimu kwa wazazi ili kuwasaidia kuishi ndoto za watoto wao kwa kuwawezesha kupata elimu bora.

Meneja huyo alitoa rai pia kwa wazazi kutumia elimu inayotolewa na Benki ya CRDB kuwawekea akiba watoto wao kwa kuwa itasaidia kuweka msingi bora katika elimu.

HABARI MICHEZO

# AZAM FC, SINGIDA ZAJIPANGA KUNUNUA TIMU ZA WANAWAKE

**Na Saada Akida**

ILI kukidhi sifa ya kushiriki mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Klabu za Azam na Singida Big Stars, zinatarajia kufanya mchakato wa kununua timu za wanawake, imeelezwa.

CAF ilitoa mwongozo unaozitaka timu zinazoshiriki mashindano yake kuanzia msimu wa 2023/24 lazima iwe na timu ya wanawake inayoshiriki mashindano yoyote katika nchi inayotokana na waraka huo umesisitizwa kuelekea maandalizi ya msimu ujao wa michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika.

Taarifa kutoka CAF imesema hadi kufikia Juni 30, mwaka huu, itakuwa mwisho wa kutoa leseni kwa timu zinazoshiriki mashindano yake na kwa hapa nchini, tayari Yanga na Simba wanauhakika wa kupata leseni hiyo kwa sababu wana klabu za wanawake.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Singida Big Stars, Ibrahim Mirambo, alisema taarifa ya CAF wameiona na wanafanyia kazi ili kuhakikisha wanamiliki timu ya wanawake na hatimaye kupata leseni ya kushiriki michuano ya kimataifa.

Mirambo alisema mchakato wa kununua timu umeshaanza na wanahitaji kupata klabu ambayo itakuwa inashiriki Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania au Ligi ya Mabingwa wa Mikoa.

"Tumeanza kufuatilia, tutahakikisha kabla kufika hiyo tarehe husika, tutakuwa tumeshapata timu, hatuna mashaka kwa sababu tayari tuna timu ya mkoa ambayo tunamiliki na kama itakuwa ni lazima tuwe na klabu ya Ligi Kuu ya Wanawake, basi tutalazimika kununua timu nyingine kutoka katika daraja hilo," alisema Mirambo.

Taarifa za ndani zinasema Azam imeanza mchakato wa kuinunua Baobab Queens ya Dodoma ambayo kabla ya kuanza kwa msimu uliomalizika iliweka kambi yake kwenye hosteli zilizopo Azam Complex, Chamazi.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Azam, Abdulkarim Amin 'Popat', alisema wako katika mchakato wa kupata timu ya wanawake ili kufanikisha vigezo vilivyowekwa ili kushiriki michuano hiyo ya kimataifa.

Mkurugenzi wa Mashindano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Salum Madadi, amesema inaruhusiwa klabu kuingia udhamini au ubia klabu nyingine na kuitumia, huku akisema huko mbele ya safari hata kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, timu zitatakiwa kuwa na timu za wanawake.



Wachezaji wa timu za vijana za umri chini ya miaka 17 wakichuana katika mechi ya Ligi ya TFF (U-17), iliyochezwa mapema wiki hii kwenye uwanja wa shirikisho hilo ulioko Kigamboni, Dar es Salaam. Pan African ilishinda mabao 3-1.
**PICHA: TFF**

# Pawasa: Simba inahitaji mastraika

**Na Saada Akida**

NAHODHA na beki wa zamani wa Simba, Boniface Pawasa, ameutaka uongozi wa klabu hiyo kutumia vyema dirisha kubwa la usajili ili timu yao irejee katika ushindani wanaoutarajia.

Simba imemaliza misimu miwili bila kubeba taji lolote lakini pia ikiishia hatua ya robo fainali katika michuano ya kimataifa kwa misimu mitatu.

Pawasa alisema Simba inatakiwa kusajili wachezaji wenye viwango bora ambao watakidhi mahitaji ya timu.

Beki huyo alisema kwa sasa Simba ipo mahali ambapo hawastahili jambo ambalo linapingana na ukubwa waliokuwa nao.

"Bidhaa ya Simba ni ubora wa kikosi chao na siyo majengo, jezi nzuri au uwanja mafanikio ya timu ni matokeo ya uwanjani, hapo utaona mashabiki wanajaa uwanjani na makombe yanatua kila msimu.

Lazima kufanya usajili wa wachezaji bora na viwango vizuri ili kuleta matokeo mazuri na kufanikisha mipango ya klabu ya kutwaa mataji ya ndani na kucheza fainali ya Afrika kama ilivyo Yanga yanatimia," alisema Pawasa.

Aliongeza anaamini katika usajili wao wangeangalia eneo la beki wa kati, kiungo mkabaji na kuimarisha zaidi katika idara ya ushambuliaji kwa kupata mastraika wenye viwango sahihi.

## Bodi ya Ligi Bara yakusanya maoni

**Na Adam Fungamwango**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), imefungua rasmi dirisha la kupokea maoni ya maboresho ya kanuni za Ligi Kuu Bara, Ligi ya Championship na First League kwa ajili ya maandalizi ya kuelekea msimu wa 2023/2024.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya bodi hiyo imesema wamefungua dirisha hilo kwa ajili ya kuandaa na kutengeneza kanuni zitakazotumika katika msimu ujao.

"Bodi imekuwa na utaratibu wa kukusanya maoni kutoka kwa wadau wa mpira wa miguu hususani ligi hizo tatu ili kupata mawazo mapya ya namna ya kuendelea kuboresha uendeshaji na usimamozi wa ligi," ilisema taarifa hiyo.

Imewataka wadau ambazo ni pamoja na mashabiki, wanahabari, vyama vya mpira wa miguu, wadhamini, taasisi za kiserikali na binafsi kutuma maoni yao kupitia barua pepe Maoni@ligikuu.co.tz, kabla ya saa 5:59 usiku ifikapo Juni 30, mwaka huu.

## Watanzania wanne kushiriki Paralimpiki

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji wanne wa Timu ya Taifa ya watu wenye ulemavu kitaondoka nchini kwenda kushiriki Mashindano ya Paralimpiki yatakayofanyika Septemba 3, mwaka huu nchini Ghana.

Akizungumza na gazeti la Nipashe Dar es Salaam jana, Makamu wa Rais wa Kamati ya Paralimpiki Nchini (TPC), Vincent Kaduma, alisema Tanzania itawakilishwa na wanariadha wawili na wanyanyua vitu vizito wawili.

Kaduma alisema kwa mara ya kwanza mchezo wa mpira wa miguu umechaguliwa kuwa miongoni mwa michezo itakayochezwa siku hiyo.

"Tunafanya mpango wa kuzungumza na BMT (Baraza la Michezo la Taifa), pamoja na Wizara kama itawezekana timu yetu ya mpira wa miguu iwe miongoni mwa timu zitakazokwenda Ghana kwa sababu imekidhi vigezo vya kushiriki michuano hiyo," alisema Kaduma.

Mwenyekiti huyo alisema wanatarajia mashindano kutokana na kushirikisha mataifa yenye wachezaji wazoefu lakini pia wanawaomba wadau kuwaunga mkono wanamichezo wetu watakaokwenda kupeperusha bendera ya nchi.

## ZISIKUPITE

### MIN-JAE KUTUA UNITED

BEKI wa Timu ya Taifa ya Korea Kusini, Kim Min-jae, mwenye umri wa miaka 26 anakaribia kujiunga na Manchester United kwa mkataba wa miaka mitano kutoka Napoli. (N***icolo Schira)***

### NEWCASTLE, UNITED VITANI

KLABU ya Newcastle United inaweza kuteka mpango wa Manchester United baada ya kufanya mazungumzo na Kim Min-jae, ambaye ana kipengele cha kununuliwa kwa pauni milioni 42 ambacho kitaanza kutumika Julai Mosi, mwaka huu. ***(Sun)***

### VILLA MACHO KWA MAGUIRE

KLABU ya Aston Villa imeonyesha nia ya kumsajili beki wa Manchester United na Timu ya Taifa ya England, Harry Maguire, mwenye umri wa miaka 30 msimu huu wa joto. ***(Football Insider)***

### TORRES ANUKIA VILLA

ASTON Villa pia wamewasilisha rasmi ofa ya kumsajili beki wa Villarreal na Timu ya Taifa ya Hispania, Pau Torres, mwenye umri wa miaka 26. ***(Mirror)***

### BAYERN YAMFUATA KANE

KLABU ya Bayern Munich bado ina matumaini ya kumshawishi mshambuliaji wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane, mwenye umri wa miaka 29 kujiunga nao licha ya kutakiwa na Real Madrid. ***(Athletic)***

### GVADIOL AKARIBIA CITY

KLABU ya Manchester City iko tayari kumtafuta mlinzi wa RB Leipzig, ambaye ni raia wa Croatia, Josko Gvardiol, mwenye umri wa miaka 21. ***(90min)***

### MESSI AWAKATAA WAARABU

KLABU ya Al-Hilal ilifanya jaribio la mwisho kumsajili mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi, kwa kumpa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35 euro milioni 500 kwa msimu. (H***elena Condis Edo)***

### KANTE ATUA SAUDIA

KIUNGO wa kati wa Chelsea na Ufaransa, N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 32, amekamilisha vipimo vya afya baada ya kukubali kujiunga na Al-Ittihad kwa mkataba wa miaka miwili wenye thamani ya euro milioni 100 kwa msimu. ***(Guardian)***

### DE GEA: SIENDI SAUDIA

GOLIKIPA wa Hispania na Manchester United, David de Gea, mwenye umri wa miaka 32 hana nia ya kujiunga na klabu ya Saudi Arabia. ***(Talksport)***

### LOFTUS-CHEEK SOKONI

AC Milan bado imeonyesha nia ya kumsajili kiungo wa England, Ruben Loftus-Cheek, mwenye umri wa miaka 27, huku mazungumzo yakiendelea kuhusu uwezekano wa kuhama kutoka Chelsea. ***(Football Insider)***

### BALOGUN AGOMBEWA ITALIA

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Folarin Balogun, ananyatiwa na AC Milan na Inter Milan, huku Mmarekani huyo mwenye umri wa miaka 21 akitarajiwa kuondoka msimu huu wa joto baada ya kucheza kwa mkopo Reims. ***(Mail)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI ATAJA SABABU KUSAJILIWA MAREKANI

● ● ● Asema uamuzi wake umezingatia maslahi ya familia na hakutaka...

**MIAMI, Marekani**

LIONEL Messi ameamua kuweka mustakabali wake mikononi mwake na kutotaka kujirudi kwa kile kilichotokea wakati anaondoka Barcelona miaka miwili iliyopita, baada ya kufichua atajiunga na Inter Miami CF inayoshiriki Ligi Kuu ya Marekani (MLS).

Messi mwenye umri wa miaka 35 aliondoka Barca Agosti, mwaka 2021 kama mchezaji huru, na kusaini Paris Saint-Germain kwa sababu vigogo hao wa Hispania hawakumudu kusajili mkataba wake ndani ya kikomo cha matumizi kilichowekwa na Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Barca walikuwa na nia ya kumrejesha mshindi huyo wa Ballon d'Or mara saba msimu huu wa joto, huku Kocha, Xavi Hernandez akithibitisha hilo. Hata hivyo, kwa mara nyingine hawakuwa na uhakika kama kanuni za ligi zitawaruhusu kusajili wachezaji wapya.

"Nilitaka sana kurudi," alisema Messi akiiambia Diario Sport baada ya kutangaza kuhamia Miami.

"Lakini, kwa upande mwingine, baada ya kuishi maisha yangu, baada ya kutoka, sikutaka kupitia hali kama hiyo tena na kusubiri kuona nini kitatokea, sikutaka kuacha maisha yangu ya baadaye mikononi mwa wengine.

"Nilitaka kufanya uamuzi wangu mwenyewe na familia yangu. Ingawa nilisikia (kwenye vyombo vya habari) Laliga ilikuwa imekubali kila kitu na kila kitu kilikuwa sawa kwangu kurudi, bado kulikuwa na mambo mengine mengi.

"Nilisikia walipaswa kuuza wachezaji au kupunguza mishahara ya wachezaji na sikutaka kupitia hilo, wala kuwajibika au kuwa na uhusiano wowote na hayo yote.

"Nilipolazimika kuondoka, walisema pia LaLiga imekubali kila kitu, lakini mwishowe haikuwezekana. Niliogopa jambo hilo hilo lingetokea tena na ningelazimika kuharakisha uamuzi wangu."

Messi alikuwa amekubali kuongezewa mkataba mwaka, 2021, lakini ilipoibuka wiki moja kabla ya msimu Barca hawakuwa na uwezo wa kusajili mkataba huo na LaLiga, ilimbidi kutafuta suluhu haraka mbali na klabu hiyo ambayo alikuwa amekaa kwa miaka 20.

Aliishia kujiunga na PSG, ambako alishinda mataji mfululizo ya Ligue 1, lakini kando na kushinda Kombe la Dunia akiwa na Argentina, alisema miaka miwili iliyopita ilikuwa migumu.

"Ilinilazimu kuja Paris, kukaa hotelini kwa muda mrefu na familia yangu, watoto wangu wakienda shule na bado nikiwa hotelini," alisema Messi.

"Hatukuwahi kutaka kuja Paris. Ilikuwa ngumu sana, sana, sana, lakini familia inaniunga mkono na ni uamuzi wa pamoja, sio wangu tu. Kuna hali ya huzuni kwao sasa, kwa sababu ilikuwa ngumu kwao mwanzoni, sasa wamezoea zaidi Paris.

"Lakini nimekuwa na miaka miwili tu ambayo mambo hayakuwa mazuri kwa familia na sikufurahia. Nilikuwa na furaha sana tuliposhinda Kombe la Dunia, lakini mbali na hayo, imekuwa ngumu sana kwa wakati kwangu Paris."

Messi pia alikuwa na ofa kutoka Saudi Arabia na klabu nyingine za Ulaya, lakini alisema wazo la kucheza MLS ndilo lilikuwa kichwani mwake.

"Nilikuwa na ofa kutoka kwa timu nyingine ya Ulaya, lakini hata sikuitathmini kwa sababu Ulaya wazo langu lilikuwa ni kwenda Barcelona tu," alisema.

"Pia niko katika wakati ambapo ninataka kutoka nje ya uangalizi kidogo, kufikiria zaidi kuhusu familia yangu.

"Baada ya kushinda Kombe la Dunia na kutorejea Barca, ulikuwa wakati wa kwenda kwenye Ligi ya Marekani kujionea soka kwa njia tofauti na kufurahia maisha ya kila siku, kwa uwazi na jukumu sawa na nia ya kushinda. "

## HABARI MICHEZO



# MADRID YAFANIKIWA KUMNASA BELLINGHAM

**MADRID, Hispania**

REAL Madrid wamefikia makubaliano na Borussia Dortmund kwa ajili ya kumsajili, Jude Bellingham, kwa ada ya awali ya euro milioni 103, klabu hiyo ya Ligi Kuu Ujerumani maarufu Bundesliga, imetangaza.

Vyanzo viliiambia ESPN mpango huo ulikubaliwa kwa karibu euro milioni 100 na nyongeza ya euro milioni 20. Dortmund ilithibitisha asilimia 30 ya ada ya awali ndio ingemaliza mkataba uliosalia.

Madrid waliwashiwa taa ya kijani kutoka kwa kinda huyo mwenye umri wa miaka 19 tangu wiki zilizopita na sasa wamechukua hatua ya mwisho kumfanya mchezaji huyo wa kimataifa wa England kuwa miongoni mwa waliosajiliwa kwenye dirisha la usajili la majira ya joto.

Madrid ilishinda ushindani kutoka kwa Manchester City, na hapo awali Liverpool, kumpata Bellingham, mmoja wa wachezaji wanaotajwa kuwa na kipaji kikubwa barani Ulaya.

Miamba hao wa Hispania wanataka kujiimarisha msimu huu wa joto baada ya kumaliza nafasi ya pili nyuma ya Barcelona kwenye Ligi Kuu Hispania (LaLiga) na kuondolewa na Manchester City katika hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Ataungana na vijana Eduardo Camavinga ambaye alisajiliwa mwaka 2021 na Aurelien Tchouameni, aliyetua klabuni hapo mwaka jana huku Madrid wakiboresha safu yao ya kiungo.

ESPN iliripoti mwezi uliopita Madrid walikuwa na matumaini ya kuwashinda City kwenye usajili huo.

Mbio za kumpata Bellingham zimekuwa kali, huku Liverpool na City zikionekana kuwa na nafasi kubwa nyakati tofauti katika msimu uliopita kabla ya Madrid kusonga mbele.

Bellingham alijiunga na Dortmund kutoka Birmingham City Julai 2020.

Katika miaka mitatu nchini Ujerumani alikua mmoja wa wachezaji bora wa Bundesliga, akicheza mechi 31 za ligi msimu huu na kufunga mabao nane, na hata kuwa nahodha wa timu hiyo.

Aliingiza England kwenye Kombe la Dunia la 2022 nchini Qatar, akianza mechi zote tano.

Madrid wamefuata sera ya kusajili vipaji wanaochipukia katika miaka ya hivi karibuni, huku Vinicius Junior, Rodrygo Goes, Federico Valverde na Camavinga sasa wakiwa wachezaji muhimu wa kikosi cha kwanza.

Pia wanatazamia kuboresha kikosi katika nafasi kadhaa, ikiwa ni pamoja na kusajili mbadala wa fowadi, Karim Benzema, aliyejiunga na Al Ittihad ya Saudi Arabia mwezi huu.

# Spurs, West Ham zamwania Maguire

**LONDON, England**

KLABU za Tottenham Hotspur na West Ham United zimepewa nafasi ya kuchunguza dili la kumsajili beki wa Manchester United, Harry Maguire, msimu huu wa joto, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30 alianza mechi nane pekee za Ligi Kuu England msimu uliopita na Kocha wa United, Erik ten Hag, yuko tayari kumwachia Maguire kuondoka katika dirisha la uhamisho.

Alipoulizwa wiki iliyopita kuhusu kutocheza kwa Maguire kwa muda Ten Hag alisema: "Nina furaha yuko hapa."

Maguire mkataba wake wa sasa hapo Old Trafford unamalizika mwaka 2025 huku kukiwa na kipengele cha kuongeza mwaka mmoja zaidi na beki huyo wa kati hapo awali amedhamiria kusalia na kupigania nafasi yake.

Hata hivyo, United iko tayari kumruhusu Maguire kuondoka katika klabu hiyo, inabakia kuonekana kama ofa thabiti kutoka kwa Spurs, West Ham au klabu nyingine itatosha kumshawishi kujaribu kufufua bahati yake kwingineko.

Spurs wanataka kuimarisha safu yao ya ulinzi msimu huu wa joto baada ya kumteua, Kocha zamani wa Celtic, Ange Postecoglou, kukinoa kikosi chao.

Ingawa Postecoglou hajaanza rasmi kazi katika klabu hiyo hadi Julai Mosi, kocha huyo mwenye umri wa miaka 57 atasaidia kuunda mipango ya uhamisho wa klabu msimu huu wa joto na jina la Maguire linatarajiwa kujadiliwa.

# Sheikh Jassim akomaa na United

**MANCHESTER, England**

SHEIKH Jassim amewasilisha ombi la tano la kuinunua Manchester United na ameiambia familia ya Glazer anataka jibu kufikia leo, vyanzo vimeiambia ESPN.

Mfanyabiashara huyo wa Qatar aliwasilisha ofa iliyoboreshwa kwa Raine Group, Benki ya Marekani inayofanya kazi kwa niaba ya Glazers, mapema wiki hii.

Vyanzo viliiambia ESPN itakuwa ya mwisho na haitakuwa sehemu ya mchakato zaidi ya leo.

Vyanzo vya habari vilisema Sheikh Jassim amechanganyikiwa zaidi kwa ukosefu wa maendeleo baada ya Glazers kutangaza mnamo Novemba, mwaka jana watazingatia "njia mbadala" ikiwa ni pamoja na uwekezaji au uuzaji kamili.

Muungano wa Qatar, unaoongozwa na Sheikh Jassim, ulitoa ofa yake ya kwanza Februari lakini sasa unataka suluhu la haraka kwa sababu una nia ya kuchukua udhibiti Old Trafford kabla ya kuanza kwa dirisha la usajili la majira ya joto Juni 14, mwaka huu.

Glazers pia wana ofa kutoka kwa bilionea wa England, Sir Jim Ratcliffe, Mwenyekiti wa Kampuni ya Kemikali ya INEOS.

Mfanyabiashara huyo anataka kununua asilimia 100 ya hisa za United huku Ratcliffe amewasilisha ofa ambayo ingemfanya amiliki 51% ya hisa huku akiwaruhusu wenyekiti wenza, Joel Glazer na Avram Glazer kuweka hisa.

Vyanzo viliiambia ESPN kwamba Glazers wametia saini harakati za United kumnunua kiungo wa kati wa Chelsea, Mason Mount, lakini kocha Erik ten Hag anazidi kuwa na wasiwasi juu ya athari ambayo uwezekano wa kuchukua nafasi hiyo kwenye mipango yake yote ya uhamisho.

Ten Hag, ambaye pia anataka angalau mshambuliaji mmoja na kipa, bado yuko gizani kuhusu ukubwa wa bajeti ya majira ya joto na amekuwa na wasiwasi kutokana na kukosekana kwa taarifa kutoka kwa bodi.

# PAZIA LA LIGI KUU BARA KUFUNGWA KIBABE LEO

**Saada Akida na Faustine Feliciane, MBEYA**

WAKATI msimu wa ligi kuu Tanzania Bara ukikamilika leo kwa michezo 15, macho ya mashabiki yapo katika vita ya kuwania tuzo ya Mfungaji Bora inayowaniwa na straika wa Yanga, Fiston Mayele na kiungo mshambuliaji wa Simba, Saido Ntibazonkiza.

Mbali na vita hiyo, kinyang'anyiro kingine kitakuwa katika hekaheka ya kujinasua kucheza mechi za 'play off', timu zilizoko kwenye hatari hiyo ni KMC, Mbeya City na Mtibwa Sugar.

Mayele mwenye mabao 16 anawania tuzo hiyo dhidi ya Ntibazonkiza aliyepachika wavuni magoli 15, na wote leo watakuwa uwanjani kuendelea na kampeni zao.

Mkongomani huyo anawania tuzo yake ya kwanza tangu aanze kucheza Ligi Kuu huku akiwa na kumbukumbu ya kuzidiwa bao moja na George Mpole aliyekuwa Geita Gold aliyemaliza katika msimu uliopita.

Yanga inashuka kwenye Uwanja wa Sokoine jijini hapa kuumana na Tanzania Prisons ikiwa na kumbukumbu ya kulazimisha sare ya mabao 3-3 dhidi ya wenyeji Mbeya City.

Ntibazonkiza ambaye timu yake inacheza na Coastal Union leo, ameibua vita hiyo ya kuwania tuzo ya ufungaji bora baada ya mchezo uliopita dhidi ya Polisi Tanzania kufunga mabao matano peke yake kwenye ushindi wa mabao 6-1.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema mchezo wa leo ni muhimu kwao kwa kuwa wanataka kumaliza ligi kwa ushindi. Kaze alisema mbio za ufungaji bora, kama Yanga wangependa kuona mshambuliaji wao Mayele anachukua tuzo hiyo kutokana na uwezo aliouonyesha katika msimu huu.

"Tunataka kumaliza ligi vizuri, tayari tumetwaa ubingwa na tuna mchezo wa fainali ya FA mbele, tunataka ushindi kwenye mchezo wa kesho (leo)," alisema kocha huyo. Naye Kocha Msaidizi wa Simba, Juma Mgunda, alisema kikosi chao kipo tayari kwa ajili ya kuwavaa Coastal Union na wanahitaji kukamilisha ligi kwa heshima huku wakifahamu wapinzani wao wanataka kujiondoa kucheza Play off.

"Mchezo hautakuwa rahisi kwa sababu Coastal Union ni timu nzuri na wamekuja kutafuta pointi muhimu, ninaimani utakuwa mchezo wa ushindani, hatutaki kupoteza pointi yeyote katika mechi yetu ya kesho (leo)," alisema Mgunda.

Naye Kocha Mkuu wa Coastal Union, Fikiri Elias, alisema wamejiandaa vizuri na wachezaji wao wako tayari kutafuta matokeo mazuri ili kujiondoa kwenye mtego wa kucheza mechi za mtoano.

"Huu ni mchezo wa kukamilisha ratiba ya msimu tunahitaji kupata matokeo mazuri ili kutocheza Play Off, lakini hautakuwa rahisi kwa sababu wapinzani wetu Simba wanahitaji kumaliza msimu kwa heshima, ila tumejianda kukabiliana nao" alisema Fikiri.

## Twiga Stars yaelekea Zambia

**Na Saada Akida**

TIMU ya Soka ya Taifa wa Wanawake (Twiga Stars), inatarajia kuondoka nchini leo na kuelekea Zambia kwa ajili ya kucheza mechi ya kirafiki ya kimataifa dhidi ya wenyeji wao She-Polopolo, imefahamika.

She-Polopolo inatarajiwa kuwakaribisha Twiga Stars katika mechi ya kirafiki ya kimataifa itakayochezwa keshokutwa mjini Lusaka.

Ofisa wa Habari na Mawasiliano wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Clifford Ndimbo, aliliambia Nipashe kikosi hicho kinatarajia kutumia mchezo huo wa kirafiki ili kujiandaa na mechi za kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa Afrika kwa Wanawake (AWCON).

Ndimbo alisema maandalizi ya safari hiyo yamekamilika na wanatarajia benchi la ufundi litautumia vyema mchezo huo wa kirafiki.

"Ni katika kuhakikisha Twiga Stars inakuwa imara kabla ya kuanza michezo yake ya kusaka tiketi ya kucheza fainali za Afrika, kupata michezo ya kirafiki ni sehemu ya programu ya Kocha Shime (Bakari)," alisema Ndimbo.



Golikipa wa Yanga, Djigui Diarra, akifanya mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Tanzania Prisons itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Sokoine, Mbeya. **PICHA: MTANDAO**

## Fei Toto kufanya makubwa

INATOKA UK. 24

Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' alisema wamedhamiria kuboresha kikosi chao kwa kufanya usajili wa wachezaji bora ambao watafanikisha timu kufikia malengo.

Popat alimtaja nahodha wao, Sospeter Bajana atabakia kikosini licha ya kuhusishwa na Simba.

## Miquissone atajwa kurejea

INATOKA UK. 24

alisema Ahmed.

Nyota huyo juzi alionekana katika video akifanya mazoezi binafsi akiwa na jezi namba 17 ya Timu ya Taifa ya Zambia (Chipolopolo), ambayo huvaliwa kiungo wa Simba, Clatous Chama.

Mashabiki wa klabu hiyo wanatafsiri hizo ni dalili kuonyesha huenda mchezahu huyo anajiandaa kurejea tena katika klabu yake ya zamani na kufanya makubwa kama ilivyokuwa awali.

Chama alimjibu kwenye akaunti yake instagram kwa maneno ya mzaha, akiandika "piga ugali mkubwa."

Tangu ajiunge na Al Ahly, mchezaji huyo amekuwa si sehemu ya kikosi cha kwanza na amekuwa akatolewa kwa mkopo kwenye klabu ya Abha FC ya Saudi Arabia.

Awali, mchezaji huyo alijiunga na Simba 2020 akitokea UD Songo ya Msumbiji, alipokuwa akiichezea kwa mkopo kutoka klabu mama ya Mamelodi Sundowns ya Afrika Kusini, lakini ilimpiga bei 2021 kwenye klabu hiyo kubwa Afrika, akiwa pamoja na Chama ambaye aliuzwa RS Berkane, lakini kwa sasa amerejea tena kwenye klabu yake ya zamani.

Wakati huo huo, taarifa zilizopatikana Dar es Salaam zinasema Bruno amekuwa katika mipango ya Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho'.

Chanzo chetu kinasema mabosi wake wa Singida Big Stars ambayo msimu ujao itashiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika wamekataa kusema chochote kuhusiana na tetesi za kuondoka kwa mchezaji wao.

"Ni mapema kusema lolote, suala la usajili linahitaji baraka ya klabu nzima, kwa sasa hakuna uamuzi wowote uliofanyika, siwezi kusema Bruno anakwenda wapo msimu ujao," kilisema chanzo chetu.

Mapema baada ya kuonyesha kiwango kizuri, kiungo huyo alionekana kuwa na dalili za kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu Bara, Yanga.

Michezo

Ijumaa Juni 9, 2023

Nipashe




**Messi ataja sababu kusajiliwa Marekani**

UKURASA 21




Mkurugenzi Mkuu wa Azam FC, Yusuf Bakhresa (kushoto), akimkabidhi kiungo mpya wa timu hiyo, Feisal Salum 'Fei Toto' jezi namba sita baada ya kutia saini mkataba wa miaka mitatu jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SAADA AKIDA**

# MIQUISSONE ATAJWA KUREJEA SIMBA SC

●●● Yumo Mbrazil Bruno ambaye pia Yanga inahitaji huduma yake baada...

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI dirisha la usajili wa wachezaji likikaribia kufunguliwa rasmi, mabosi wa Simba wamethibitisha wapo tayari kumrejesha kiungo mshambuliaji wake wa zamani, raia wa Msumbiji, Luis Miquissone, iwapo watafikia makubaliano na Al Ahly, imefahamika.

Nyota mwingine anayetajwa kuwindwa na Simba ni kiungo Brazil Bruno Gomes, ambaye amekuwa na kiwango kizuri katika msimu wake wa kwanza aliowatumikia Singida Big Stars ya mkoani Singida.

Miquissone aliondoka Simba na kujiunga na Waarabu hao baada ya kuonyesha kiwango cha juu, lakini 'Mmakonde' huyo ameshindwa kuwa na wakati mzuri huko Misri.

Akizungumza na Nipashe, Meneja wa Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema mpango huo upo na wanachosubiri ni kufahamu kiasi gani cha fedha Al Ahly itahitaji ili kutoa baraka za mchezaji huyo kurejea Tanzania.

Ahmed alisema mchakato huo hauna mashaka kwa sababu iwapo Al Ahly watataka kumuuza ni lazima wawasiliane na Simba kama walivyokubaliana wakati wanamuuza mwaka 2021.

" Luis ni mchezaji wa Al Ahly, lazima mashabiki wa Simba waelewe ana mkataba wa klabu hiyo, na makubaliano ya Al Ahly na sisi tuliyoingia ni endapo wakitaka kumuuza wanapaswa kwanza kuiambia Simba, kwa hiyo tutawasikiliza kama wanamuuza watatuambia, watatutajia na bei.

Mambo yakiwa mazuri tutafanya biashara, yote kwa yote mchezaji huyu akitua Msimbazi kila mmoja anajua balaa lake, kuhusu pesa wala hatuna matatizo kabisa msimu huu tumedhamiria, tutamsajili yoyote ambaye tutamhitaji,"

INAENDELEA UK. 23

## Fei Toto kufanya makubwa Azam FC

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kukamilisha usajili wa kujiunga na Azam FC, kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto', ameahidi kufanya makubwa ndani ya timu yake mpya katika Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa watakayoshiriki kwenye msimu ujao.

Kiungo huyo alitangazwa rasmi kujiunga na Azam FC jana kwa kutia saini mkataba wa miaka mitatu ambao utamalizika ifikapo mwaka 2026.

Fei Toto alisema kile ambacho alikifanya ndani ya klabu yake ya zamani ya Yanga pia anatarajia kukionyesha akiwa na timu yake mpya kwa ajili ya kuhakikisha wanafikia malengo yaliyotarajiwa katika msimu ujao.

Alisema anamshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan, kwa sababu agizo lake kwa viongozi wa Yanga kumaliza mgogoro limefanikiwa na hatimaye kufanikiwa kujiunga na Azam FC.

Baada ya kujiunga na Azam FC, kiungo huyo alitolea ufafanuzi kuhusu fedha alizochangisha kwa ajili ya kufungua kesi katika Mahakama ya Usuluhishi ya Kimataifa ya Michezo (CAS); "Zile pesa siwezi kuzirejesha kwa walionitumia maana ni watu wengi na sitawajua wote, kwa hiyo nitazipeleka kwa watoto yatima, msikitini na makanisani kwa watu wenye uhitaji, siwezi kuzitumia," alisema Fei Toto.

Katika hatua nyingine mabosi wa Azam wamesema wataendelea kuboresha kikosi cha timu yao kulingana na mahitaji ya benchi lao la ufundi linalonolewa na Kocha, Youssouph Dabo.

Katika maboresho hayo ni kufanya usajili mzuri kulingana na mahitaji lakini pia kuhakikisha wanawazuia kwa kuwaongezea mikataba baadhi ya wachezaji wao muhimu ili wabakie kikosini.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >